**14 JUNI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Arobaini na Nane – Tarehe 14 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu sasa namwita Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 618

**Uwekezaji wa fedha za wafanyakazi katika miradi ya kiuchumi**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, ni faida gani ambayo Wafanyakazi wanapata kupitia uwekezaji wa fedha wanazokatwa na Vyama vya Wafanyakazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ambayo wafanyakazi wanapata kupitia uwekezaji wa fedha wanazokatwa na Vyama vya Wafanyakazi ni pamoja na; Vyama vya Wafanyakazi kusuluhisha migogoro ya kikazi kwa niaba ya wanachama wake, kutoa huduma kwa wanachama kama vile ya utetezi katika Mahakama ya Kazi, na kutoa elimu kuhusu Sera na Sheria za kazi kwa ajili ya maslahi mapana ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Wafanyakazi kupitia fedha wanazokusanya kutokana na ada za wanachama wao huzitumia kutekeleza majukumu ya vyama yaliyowekwa kikatiba na kisheria yanayotokana na uwepo wa vyama mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo baadhi ya Vyama vya Wafanyakazi ambavyo hutumia ada za uanachama kujenga majengo kwa ajili ya matumizi ya ofisi za vyama, kuwapangisha watu mbalimbali na kutoa huduma kwa wanachama wao. Fedha inayopatikana kutokana na uwekezaji hutumika kuongeza bajeti za Vyama vya Wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kikatiba na kisheria kikamilifu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba fedha za wafanyakazi zinaweka uwekezaji ambao unaendelea, yaani unafanyika uwekezaji mfano kujenga majengo ambayo yanaongeza kipato kwenye Vyama vya Wafanyakazi. Ninatamani kufahamu.

Ni lini Serikali itakuja na sheria ambayo inampa haki mwanachama yule kuweza kupata gawio kwa fedha zinazopatikanika kwa uwekezaji huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Nataka kufahamu, kumekuwa na malalamiko mengi ya walimu kuhusiana

na kulazimishwa kuingia kwenye vyama viwili viwili vya wafanyakazi: Ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba kujiunga na uanachama wa Vyama vya Wafanyakazi ni hiari ili kusikuwepo na huko kulazimishana kuingia kwenye vyama viwili viwili hususan kwa walimu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda nimjibu Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini kwenye eneo hili la uwekezaji nimefafanua vizuri na sheria ipo ambayo inaviruhusu vyama hivi vya wafanyakazi, pia zipo kanuni ambazo zinawaongoza katika vyama vya kwa misingi ya katiba walizojiwekea. Kwa hiyo, nichukue tu kama maoni katika eneo hili, nitaonana naye baada ya hapa ili tuweze kuzungumza zaidi kuona nini hasa alimaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile amesema kwamba wanachama wanalazimishwa kujiunga. Niseme kwamba vyama hivi ni vya hiari, lakini Katiba zao ndiyo ambazo zinawabana kwamba pengine ujiunge au ukijiunga atanufaika na nini na kipi? Kwa hiyo, siyo kwamba ni lazima kwamba lazima sasa ujiunge kwenye chama hiki. Hapana, lakini pia nitakutana naye tufahamiane zaidi ili tuone namna ya kuliweka vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika vyama hivi ulazima upo, maana mfanyakazi hasa mwalimu anapoingia tu kwenye ajira anakatwa pesa bila yeye kuwa na ridhaa yake: Je, kama unasema siyo lazima, unaweza ukatoa tamko leo ili mwalimu yeyote aingie chama chochote anachokitaka yeye? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya awali, nimesema zipo katiba ambazo zinavi-*guide* hivi vyama, kama pengine ni cha walimu au ni chama cha kada nyingine tofauti, wapo pale kwa mujibu wa katiba zao na makubaliano ambayo wanakubaliana wao kwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu zipo baadhi ya changamoto pengine na migogoro katika vyama hivi. Serikali ya Awamu ya Sita chini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tutaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na vyama hivi kuboresha upungufu ambao upo au kusuluhisha migogoro ambayo inaendelea katika vyama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe wasiwasi walimu, waendelee kukiamini Chama chao cha Walimu na sisi Serikali tuko pamoja nao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sima swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa wafanyakazi ni mali ya Serikali na Serikali ina wajibu kwa wafanyakazi hawa.

Je, haioni sasa umefika wakati mfanyakazi halazimishwi kujiunga kwenye chama bila hiari yake? Nadhani ni muhimu sana kutoa tamko hili Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Sima. Kama ambavyo nimejibu, amesema wafanyakazi ni mali ya Serikali. Nami niseme, tunawapongeza sana wafanyakazi wa Tanzania kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii kuliletea maendeleo Taifa letu, lakini

tutaendelea kufanya mashauriano na kutoa ushirikiano na vyama hivi vya wafanyakazi ili waendelee kuwa na imani na vyama vyao na kuendelea kuliletea maendeleo. Ni mafanikio makubwa yamepatikana kupitia vyama hivi vya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaona hata Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amepandisha madaraja, ameongeza fedha, anaendelea kupigania maslahi ya wafanyakazi. Kwa hiyo, niwatoe shaka wafanyakazi, tuko pamoja na tutaendelea kuwaratibu vizuri kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais TAMISEMI. Sasa namwita Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang' aulize swali lake.

Na. 619

**Ujenzi barabara ya Mogitu – Dawar – Ziwa Chumvi**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mogitu – Dawar hadi Ziwa Chumvi ili kusafirisha chumvi ghafi kwenda kiwandani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang' kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, shilingi milioni 188.73 zimetumika kwa ajili ya kufungua na kujenga makalavati manne katika barabara ya Dawar – Ziwa Chumvi ambapo awali ilitumika kama njia ya ng'ombe (Pario).

Ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe kwenye eneo la kilometa 6.3 umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 53.34 kwa ajili ya kujenga kipande cha Barabara ya Endasak - Dawar inayoelekea Ziwa Chumvi chenye urefu wa kilometa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuihudumia Barabara ya Mogitu – Dawar mpaka Ziwa Chumvi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa fedha ambazo zimewekwa kwa ajili ya barabara ya Mogitu – Dawar – Ziwa Chumvi, lakini pia kwa shilingi milioni 53 ambayo imetengwa kwa ajili ya Dawar – Endasak. Pamoja na pongezi hizo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza maeneo ya Mara – Getaqul ambayo iko Kata ya Measkron**,** na Merekwa – Gauror ambayo iko Kata ya Dirima na Sosomega ambayo iko Kata ya Hirbadaw kipindi cha mvua huwa yanakuwa kama yako kisiwani.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka kufikisha mkono wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan maeneo hayo ili nao waweze kufurahia maisha kwenye eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tuna changamoto kubwa ya daraja kule Sirop. Serikali imeshatenga fedha shilingi milioni 568; je, ni lini ujenzi wa daraja hilo utaanza ili wananchi waachane na adha ya daraja hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hhayuma. Swali lake la kwanza hili la Kata ya Dirima aliyotaja na

vijiji ambapo barabara hizi zipo katika kata ambayo mvua ikinyesha wanakuwa wako kisiwani, naomba nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Hanang' kwenda kufanya tathmini ya barabara hii na kisha kuiwasilisha Makao Makuu ya *TARURA* ili kuona ni namna gani tunaweza tukai-*accommodate* katika bajeti zifuatazo kuitengeneza barabara hii ili wananchi hawa wasiwe kisiwani kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Hhayuma kwa sababu amekuwa akifuatilia sana upatikanaji wa fedha wa daraja hili ambalo linaenda kujengwa kwa Shilingi milioni 568 ambalo amelitaja yeye mwenyewe, nimhakikishie kwamba mara tu tutapoanza mwaka wa fedha wa 2023/2024 ujenzi huu utaanza kwa kutangaza kazi hii ili apatikane kandarasi kwa ajili ya kujenga daraja hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara ya kutoka Korongo kwenda Utinta imekuwa na changamoto kubwa sana na kuleta hatari kwa wanafunzi: Ni lini mtawaongezea fedha *TARURA* ili waweze kujenga kipande hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Serikali imeongezea fedha *TARURA* ukilinganisha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022, 2022/2023 na hata 2023/2024 tunayoenda kutekeleza, *TARURA* wameongezewa zaidi ya mara tatu ya bajeti ambayo ilikuwepo hapo awali. Kwa hiyo, ni kukaa na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa kuangalia ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kukarabati vile vile eneo la Wilaya ya Nkasi anakotoka Mheshimiwa Khenani ambapo wanafunzi wanavuka kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba vile vile Meneja wa Wilaya ya Nkasi awasilane na Mheshimiwa Khenani ili kuona ni namna gani wanaweza wakaanza ukarabati wa barabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu *DC* Barabara ya Mgombe – Kagerankanda mpaka Mvinza ni barabara ya kiuchumi na hupitisha malori makubwa kwenda kuchukua chokaa kupeleka nchi jirani ya Burundi; je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ambayo ameiulizia Mheshimiwa Genzabuke kwenye swali lake la nyongeza, ni barabara ambayo inaambaa ambaa pembezoni mwa Mto Malagarasi. Kule wanaenda kufuata *clinker* ambayo inatengenezea madini ya ujenzi *(cement)*. Kwa hiyo, tunaiona changamoto hii iliyopo kwa sababu mwanzo wakati barabara hii inahudumiwa na *TARURA* kulikuwa bado hakuna malori mengi yanayopita yenye uzito mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kwa sababu malori tayari ni mengi sana, tutakaa na wenzetu wa *TANROADS* kuona ni namna gani ambapo wao wenyewe wataanza kwanza kule Kasulu kuona ni namna gani wanapandisha hadhi barabara hii kuwa barabara ya *TANROADS* ili iweze kuhudumiwa kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwongezee tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hata Mamlaka ya Bandari Tanzania nayo ilikuwa inaangalia uwezekano wa kupanua mto ule ili zile *barge* kubwa ziweze kuwa zinapita kuchukua ile *clinker* badala ya kupitisha kwenye barabara zile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Askofu Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Kwa sababu ya wingi wa mvua zinazonyesha katika Jiji la Dar es Salaam, barabara nyingi zilizo chini ya *TARURA* katika Jimbo la Kawe zimekatika vipande vipande.

Ni nini mpango wa Serikali ku-*repair* barabara hizi ili wananchi waweze kupita na kuondoa usumbufu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gwajima la barabara za Dar es Salaam kukatikakatika kwa sababu ya mvua, tunaenda kuanza kutekeleza Bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa Wakala wa barabara ikiwemo Dar es Salaam. Mheshimiwa Mbunge naye ni shahidi kwamba hivi karibuni wamesaini mkataba kwa ajili ya uanzishwaji wa mradi wa *DMDP II* ambao utakwenda kuwa mwarobaini wa barabara hizi mbovu za Jiji la Dar es Salaam kwa kujenga mifereji na kuhakikisha barabara pia zinapitika wakati wote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 620

**Barabara ya Ninde, Masokolo mpaka Lupata**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Ninde, Masokolo hadi Lupata katika Kata ya Kuzumbi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ninde – Masokolo – Lupata yenye urefu wa kilometa 40 inahudumia vijiji vitatu ambavyo ni Ninde, Masokolo na Lupata. Barabara hii ipo mpakani mwa Tanzania na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo ni muhimu kwa shughuli za kufuatilia masuala ya kiusalama. Barabara hii haipo kwenye mtandao wa barabara za *TARURA*. Hivyo, barabara hiyo inahitaji kufunguliwa ili kuunganisha vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafungua barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuimarisha usafiri na usafirishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vincent, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Vijiji vya Lusembwa, Ng'undwe, Mlambo, Minza na Ifinga vinashindwa kupata huduma ya maji, miradi ya maji, mawasiliano pamoja na minara ya simu.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara katika hivi vijiji ambavyo viko Kata ya Wampembe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kata ya Wampembe na Kata ya Kala kuna vilima ambavyo ni korofi, vinasababisha magari ya abiria kutopita; je, ni lini Serikali itajenga kwa zege katika vilima hivi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbogo, la kwanza, hii barabara ya Ng'undwe – Mlambo – Lusembwa – Mvinza na Ifinga vilivyokuwepo kwenye Kata hii ya Wampembe, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, barabara hizi zilikuwa bado hazijafunguliwa na kuingizwa kwenye mtandao wa *TARURA*. Hivyo basi, muda siyo mrefu Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Nkasi atapita kufanya tathmini ya barabara hizi na kuona ni kiasi gani kinatakiwa kutengwa ili barabara hizi ziweze kuchongwa na greda, na kadiri miaka inavyoenda na fedha kuruhusu basi nazo ziweze kuanza kuwekewa changarawe ili wananchi waweze kupita wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili kuhusu barabara inayounganisha Kala na Wampembe, kwamba ina vilima vingi, nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Nkasi, kuweza kufika katika barabara hii ya Kala na Wampembe na kuanza tathmini, na kuona ni kiasi gani kinahitajika kwa ajili ya kuweka zege katika vilima hivi ili barabara hizi ziweze kuwa zinapitika wakati wote wa mvua na hata kipindi ambacho hakuna mvua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Songe, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Barabara ya kutoka pale Nyasho kupitia Mwanangi – Badugu kwenda Busami imekuwa ikiharibika mara kwa mara na ni ya muhimu sana katika uchumi wa Jimbo la Busega: Je, lini Serikali iko tayari kujenga barabara hii kwa kiwango cha changarawe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa Songe la barabara zake kule Jimboni Busega, wote ni mashahidi kwamba *TARURA* sasa imeongezewa fedha mara tatu na Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani,

na bajeti ile imebaki pale pale katika kiwango cha juu cha zaidi ya Shilingi bilioni 776 ambayo Bunge hili lilipitisha. Hivyo basi, niwatoe hofu Wabunge wengi kwamba sasa tunakwenda kufungua barabara nyingi zaidi za mijini na vijijini na vile vile kukarabati barabara nyingi zaidi zikiwemo za kule kwa Mheshimiwa Songe Wilayani Busega.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara ya kutoka Liweta mpaka Mpopoma ni barabara ambayo ni muhimu sana kiasi kwamba inatenga hicho kijiji kuwa katika mawasiliano na Wilaya ya Nyasa ambayo ndiyo wilaya yake.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kipekee kuisaidia barabara hii ambayo pia ina milima kama ilivyo barabara ya Wampembe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Stella Martin Manyanya la barabara hii ambayo inapita Liweta – Mpopoma kule Wilayani Nyasa, nayo vilevile nichukue nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Nyasa kwenda kwenye barabara hii aliyoitaja Mheshimiwa *Engineer* Manyanya na kuifanyia tathmini na kuona ni kiasi gani kitahitajika kwa ajili ya kuweza kujenga ili tuweze kutengea fedha katika miaka ya fedha ambayo inafuata.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 621

**Ahadi ya ujenzi wa barabara ya lami – Mombo**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga barabara za lami katika Mji wa Mombo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, *TARURA* ilitenga jumla ya kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuchonga na kuweka changarawe urefu wa kilometa 2.7, kujenga makalavati tisa, kujenga mifereji yenye urefu wa kilometa 1.9. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuchonga kilometa 2.84 kwa kuweka changarawe, ujenzi wa makalavati 23 na ujenzi wa mifereji urefu wa kilometa 2.46. Utekelezaji wa kazi hizi unaendelea na umefikia asilimia 56. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili ya barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Mombo Mjini zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami mara baada ya kuziimarisha kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa mifereji kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ujenzi wa barabara za lami kilometa tatu kwenye Mji wa Mombo ni ahadi ya Serikali iliyotolewa na Mgombea wa Urais wa Chama cha Mapinduzi mwaka 2015 na ikarejewa mwaka 2022. Kazi inayoendelea haiathiri ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, nataka kujua, ni lini ahadi hii ya Serikali kwenye Mji wa Mombo itatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wilaya ya Korogwe ni eneo muhimu sana kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo, kilimo cha mkonge lakini Tarafa ya Bundi kilimo cha chai: Ni lini Serikali itaiingiza Wilaya ya Korogwe kwenye mradi ule mahususi wa miundombinu kwenye maeneo ya uzalishaji na maeneo ya kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, la kwanza hili kwamba barabara hii ya lami ni ahadi ya Serikali, nikiri kwamba ni ahadi ya Serikali na kwamba tutaendelea kuipa kipaumbele kwa sababu iliahidiwa na Kiongozi Mkuu wa Nchi alipopita katika eneo la Mombo. Tutaendelea kutafuta fedha na tutaona ni namna gani katika mwaka wa fedha huu tunaoenda kuuanza ni nini kinaweza kikafanyika na Serikali kuweza kuendelea kutekeleza ahadi hii ya viongozi wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili kwamba kule kuna uzalishaji mkubwa kuingiza katika miradi mbalimbali mingine, nimtoe mashaka, Korogwe vijijini ipo katika mradi ule wa *bottleneck removal* ambao unakwenda kujenga madaraja na vivuko mbalimbali katika maeneo tofauti hapa nchini, ikiwemo kule kwake Mheshimiwa Mnzava, Korogwe Vijijini. Najua alichokuwa anataka ni kwamba Mkoa wa Tanga wawekwe katika Mradi wa *Agri-connect,* lakini mradi huu wa *Agri-connect* upo katika *Southern Highlands,* mikoa yetu ya nyanda za juu kusini tu, na wao Korogwe wapo katika hii *bottleneck removal* kwa vijijini; kwa Korogwe Mjini, kwa Dkt. Kimea kule, wamo katika *TACTIC* na Tanga Mjini vile vile wapo katika *TACTIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara mbalimbali kule Korogwe Vijijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami ninalo swali linalofanana na Korogwe. Pale Mji wa Nguruka Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliwaahidi kilometa tano za lami, lakini mpaka sasa zimejengwa mita 250 tu. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga barabara za lami pale Nguruka? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon kwenye hii barabara ya Nguruka ambayo ni ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutakaa kupitia ahadi zote za Viongozi Wakuu, kupitia wakala wetu wa *TARURA* na kuona ni namna gani tunaweza tukakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuona tunapataje fedha ya kuanza kutengeneza taratibu kutenga ili kila mwaka angalau kwenye ahadi hizi tuweze kuwa tunapunguza kilometa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunalifanyia kazi chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Angellah Kairuki, kuhakikisha kwamba tunajua ahadi zote na kuziratibu na kuhakikisha barabara hizi zinajengwa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPEHT N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara ya Vwawa – London – Iganduka hadi Msiya hivi sasa haipitiki kabisa; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha

kwamba barabara hiyo inawekwa lami ili iweze kupitika wakati wote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa Hasunga la Barabara zake hizi za Vwawa kuwekewa lami. Nitakaa naye Mheshimiwa Hasunga kuona ni kiasi gani kimetengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 katika jimbo lake kule ili tuweze kuhakikisha kwamba upatikanaji wa fedha huu unakuwa wa haraka na hizi ziweze kuanza kujengwa mara moja na kama hazijatengewa fedha basi tutahakikisha na Mheshimiwa Hasunga tutakaa naye kuona zinatengewa fedha katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Ishengema swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, je lini Serikali itajenga Barabara ya Mikumi, Kisanga, Maroro kwa kiwango wa changarawe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itajenga Barabara hii ya Mikumi, Kisanga kama ambavyo ameuliza Dkt. Ishengoma kadiri ya upatikanaji wa fedha na tutaangalia katika mwaka wa fedha huu unaoanza, ambapo *TARURA* vile Bunge hili lilipitishia bajeti kubwa ya kuweza kutekeleza barabara hizi kuona kama imetengewa fedha na kama haijatengewa fedha tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata ili barabara hii iweze kutengewa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Awack swali la nyogeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kilometa 10 katika Mji wa Karatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakaa naye Mheshimiwa Mbunge kwa sababu bado sijaelewa ahadi hii ilikuwa iko vipi. Nitakaa naye Mheshimiwa Mbunge ili aweze kunielewesha vizuri ahadi hii ya kilometa 10 ilikuwa ni ahadi ipi na tuweze kujua kama ni ya *TANROADS* au ni ya kwetu halafu tuone ni namna gani tunaweza tukapata fedha ya kuanza kutekeleza walau kwa kilometa moja moja ili iweze kukamilika kule Karatu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka litaulizwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 622

**Uhitaji wa fedha za kumalizia Vituo vya Afya vya Matwiga na Mafyeko – Chunya**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K. n. y MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya Matwiga na Mafyeko Jimboni Lupa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 na 2021/2022 Serikali ilitenge kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Isangawana katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati nchini kote ikiwemo ukamilishaji wa vituo vya afya vya Matwiga na Mafyeko katika Halmashauri ya Chunya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa niaba ya Mheshimiwa Masache nashukuru sana Serikali kwa majibu mazuri na tunaamini wananchi wa Lupa kwenye mgawanyo wa magari watapata. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza lini Serikali itapeleka fedha za kumalizia ujenzi wa kituo cha afya Masamakati na Mkwansira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili wananchi wa Kata ya Rom pamoja na ufinyu wa maeneo wamehangaika sana wamepata eneo la kujenga kituo cha afya pale Rowsinde. Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasaka yaliyoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mbunge wa Hai rafiki yangu Saashisha Elinikyo Mafuwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza la lini Masamakati itapelekewa fedha? Naomba nijibu haya maswali mawili kwa pamoja hili la kwanza na la pili. La kwanza ni kuwataka wao Halmashauri ya Wilaya ya Hai kuanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya vya Rowsinde na hichi ambacho cha Masamakati. Pale watakapokuwa wanakwenda na kukitengea fedha katika bajeti zao ndipo napo Serikali wakati tunatafuta fedha ya kuendelea kujenga vituo vya afya, tunaona ni namna gani tutakuja kuongeza nguvu za halmashauri walikofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya awamu ya sita ya mama Samia Suluhu Hassan imejenga vituo vya afya 234 kote nchini kwa kutenga bilioni 116 na tayari vituo hivyo vingi vimeshakamilika na kuanza kazi. Sasa ni wajibu wa halmashauri hizi nazo ku-*support* jitihada hizi za Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuweka fedha kwa ajili ya ujenzi huu kwa wao kuanza ujenzi wa vituo hivi vya afya. Naamini kule wenzetu wa Hai nao watakaa halmashauri na kuweka fedha kwa ajili ya kuanza kupeleka huduma ya wananchi huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kumwelekeza Mganda Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwenda kufanya tathmini katika maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Saashisha na kuona idadi ya wananchi waliokuwepo pale, uhitaji uliopo kwa ajili ya kupata vituo hivi vya afya na kuwasilisha taarifa ile Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Tarafa ya Mlalo yenye kata nne inahitaji kituo kimoja cha kimkakati ambacho kitahudumia Kata ya Lukozi, Malindi, Manolo na Shume.

Je, Serikali ina mpango gani kujenga kituo hiki kwa haraka kwa sababu pia ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Kata ya Lukozi?

**MWENYEKITI:** Naona amesimama Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Angelah Kairuki majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nipende kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru kwa namna ambavyo ameendelea kufuatilia maendeleo ya jimbo lake lakini kwa namna ambavyo ameendelea kufatilia utekelezaji wa ahadi za viongozi wetu. Nipende tu kumwakikishia kwamba tunatambua umuhimu na namna ambavyo Kata hii ya Lukozi iko

kimkakati. Tunajua kituo hichi endapo kitajengwa kitaweza kuhudumia zaidi ya kata nne ikiwemo Manolo, Malindi, Lukozi yenyewe na nimpe tu uhakika. Kwamba tutakijenga katika mwaka ujao wa fedha 2023/2024 kama ambavyo tutaweza kupanua Kituo cha Afya cha Mlalo vilevile katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa Mheshimiwa Shekilindi tutaweza pia nako kujenga kituo cha afya kwa upande Gare, nikushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa mimi ruhusa ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Chitage na Kata ya Usagari Mbunge kwa kushirikiana na wananchi tunajenga vituo vya afya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia kumalizia vituo hivyo vya Chitage na Usagari Mikungumalo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Almas Maige yeye pamoja na wananchi wake kuweza kujitoa kuanza ujenzi wa vituo hivi vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nimtake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora kufika katika vituo hivi vya afya ambavyo vimeanza kujengwa kwa nguvu ya wananchi na kufanya tathmini na kuona vile vigezo ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kusajili kituo cha afya kama wanakidhi hawa wananchi wa Mheshimiwa Maige na wawasilishe taarifa hiyo Ofisi ya Rais TAMISEMI ili tuviweke katika mipango yetu ya utafutaji wa fedha katika Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona, wananchi wa Mji wa Mafinga walishaanza kujenga Kituo cha Afya cha Upendo na kwa nguvu zao wenyewe.

Ni lini Serikali itapeleka nguvu za ujenzi katika kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka fedha katika Kituo hicho cha Afya Upendo ku-*support* nguvu za wananchi kadiri ya upatikanaji wa fedha. Vilevile nao wana uwezo wa kuanza kutenga bajeti kwa ajili ya ku-*support* jitihada hizi za wananchi hawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aisharose Matembe swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Je, lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kumalizia Kituo cha Afya cha Makuro Jimbo la Singida Kaskazini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka fedha za kumalizia Kituo cha Afya Makuro kadiri ya upatikanaji wa fedha na tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona kama kimetengewa fedha katika mwaka wa fedha ujao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magessa swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye Kata za Rwamgasa, Nyakagomba na Magenge tulizoziomba mwaka 2021?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itajenga vituo vya afya hivi alivyovitaja Mheshimiwa Magessa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo Mbunge wa Mbagala sasa aulize swali lake.

Na. 623

**Hatma ya kipande cha barabara kutoka Zakhiem – Mbagala Kuu**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, nini hatma ya Barabara ya Zakhiem Mbagala Kuu inayoshindwa kujengwa kwa kuwa bomba la mafuta lipo chini ya barabara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kijichi - Mbagala Kuu - Zakhiem ina urefu wa kilometa 5.1. Kati ya kilometa hizo kipande cha mita 600 ni sehemu ya bomba la mafuta la TAZAMA. Baada ya majadiliano ya mara kwa mara kati ya *TARURA*, TAZAMA na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, *TAZAMA* waliruhusu mita 200 kuwekewa tabaka la zege na tayari tabaka la zege limewekwa kwa gharama ya shilingi milioni 155.79 kupitia mradi wa *DMDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipande cha mita 400 kilichobaki, *TAZAMA* wameruhusu kiwekewe tabaka la

changarawe pekee na sio kujenga barabara kwa kiwango cha lami au zege.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa barabara na kwa kuwa nyumba zilizo mbele ya Barabara hii, viwanja vyake vilipimwa na mamlaka ya upangaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufidia walau mita sita ili wananchi wa eneo hili wapate Barabara ya uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili nini hatma ya barabara ya Mabwawa ya Samaki na Mlima habarizenu iliyopo katika Kata ya Mianzini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Chaurembo. La kwanza hili la kipande cha mita 400 kilichosalia katika barabara hii ya Zakhiem.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii kwa kumbukumbu zangu ni barabara ambayo inaunganika na maandazi *road* ambayo barabara hii ya *Maandazi Road* imewekwa katika mpango wa *DMDP II.* Sasa kwa sababu ni mita chache kutoka pale tutakaa na wenzetu wa Manispaa ya Temeke na vilevile tutakaa na wenzetu wa *TARURA* Mkoa wa Dar es Salaam kuona ni namna gani tunaweza tukachepusha barabara hizi mita 200 kwa kuona kama tunaweza kuingiza katika mpango wa kulipa fidia. Halmashauri wenyewe baada ya kufanya tathmini walipe fidia kwa ajili ya kuchepusha barabara hii ili iweze nayo kuingizwa katika mipango ya kuwekewa lami au zege ili wananchi hawa waweze kupata huduma sahihi wanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili, barabara hii aliyoitaja ya Bwawa la Samaki hadi Kilima cha

Habaribzenu. Naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kufika katika barabara hii na kuweza kufanya tathmini na kuona ni namna gani inaweza ikatengewa fedha ya kuweza kutengeneza ili iweze kupitika wakati wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry Silaa swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Mvua za masika zimekuwa ni ndefu sana kwenye Mkoa wa Dar es Salaam na miundombinu mingi ya barabara imeharibika. Tarehe 30 Mei Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kwamba Barabara ya Banana-Kitunda-Kivule - Msongola itapitika na hali bado ni mbaya ikiwemo Barabara ya kwa Diwani – Bomba mbili. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na miundombinu hii ya Jimbo la Ukonga ambayo ina hali mbaya kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry William Silaa naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Dar es Salaam aweze kutembelea barabara hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa Jerry William Silaa na kufanya tathmini ya haraka na pale tunapoanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuzipa kipaumbele barabara hizi kwa ajili ya kuzitengeneza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana swali langu ni dogo tu kusiana kama lililokuwa Mbagala. Iko barabara inayopita ndani ya Jimbo la Temeke, sawa sawa na sambamba na Reli ya *TAZARA* ambayo nayo katika mvua hizi imeharibika sana.

Je, Serikali mtatusaidiaje changamoto ya *TAZARA* pamoja na Manispaa yetu ili waturuhusu hata kuitengeneza tu kwa

changarawe au hata kuweka lami kidogo kwa sababu ni Barabara ambayo inatumika sana kwa wananchi wa Temeka na hasa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeeleweka hapo, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii alimradi inapita kandokando mwa reli kuna sheria ambazo zinalinda ile mipaka ya reli inakopita. Hivyo tutakaa na wenzetu wa *TAZARA* kuona ni namna gani wataruhusu ipitike kwa muda kwa sababu haitoweza kutengenezewa miundombinu kama ya zege na lami kwa muda ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi na *TAZARA* wakiridhia basi tutaona ni namna gani Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Dar es Salaam anaweza akatengea fedha kwa ajili ya kuweza kuweka changarawe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafsi niulize swali la nyongeza. Je, lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Ilula, Ibumu ili ijengwe japo kwa kiwango cha changarawe tu na madaraja manne ili wananchi waweze kupita, manake sasa hivi wanapata mateso makubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakaa na Mheshimiwa Kabati kuona kama barabara hii ya Ilula - Igumu imewekwa katika mradi wa Agri-*connect* ambao wao Iringa ni wanufaika wa mradi huu. Kama haijawekwa basi kuona ni namna gani bajeti ya *TARURA* ya Wilaya ya Kilolo inaweza ika-*accommodate* barabara hii katika mwaka wa fedha unaofuata na kama sio mwaka wa fedha unaofuata basi ule wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate Mbunge wa Kyerwa sasa aulize swali lake.

Na. 624

**Kuwapandisha watumishi vyeo kwa mserereko – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuwapandisha vyeo kwa mserereko kufikia daraja wanalostahili watumishi waliosubiri zaidi ya miaka 8 Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishwaji vyeo kwa mserereko ni utaratibu unaotumika kuwapandisha vyeo watumishi ambao imethibitika kuwa walicheleweshwa kupandishwa vyeo kwa wakati kwa kuzingatia miongozo ya upandishaji vyeo iliyopo, uwepo wa nafasi iliyoidhinishwa katika Ikama na uwepo wa fedha za kugharamia upandishwaji vyeo kwenye bajeti, sifa za kielimu na kitaaluma na utendaji kazi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa maelezo hayo, Serikali itakuwa tayari kuwapandisha vyeo kwa mserereko watumishi waliotajwa na Mheshimiwa Mbunge endapo itathibitika kuwa wana sifa zilizoainishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Sebba swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nishukuru Serikali kwa majibu yake. Wilaya ya Kyerwa tunayo mapungufu ya watumishi kwenye sekta ya elimu pamoja na sekta ya afya.

Je, lini Serikali itaongeza watumishi kwenye sekta hizo ambazo nimezitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuna watumishi 18 ambao wamestaafu mwaka 2018 wakiwemo watendaji wa kata, watumishi hawa mpaka sasa hivi bado hawajalipwa mafao yao. Nini tamko la Serikali juu ya watumishi hawa kulipwa mafao yao ili na wao waweze kufurahia utumishi ambao wametumikia Taifa hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba Serikali imeendelea kupandisha madaraja watumishi wake pia imeendelea kuajiri watumishi katika maeneo ambayo yanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu aliyoyaeleza Mheshimiwa Mbunge nataka nimwahidi kwamba Serikali imeendelea kuyashughulikia na kwa mfano katika bajeti iliyopita ya mwaka 2022/2023 vibali vya ajira 30,000 vilitolewa na watumishi wote hawa waliajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka unaofuta wa fedha ambao Bunge lako limetupitishia bajeti yetu tunatarajia kuajiri wafanyakazi au watumishi 45,000. Nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba Serikali itaendelea kukabiliana na upungufu wa watumishi katika sekta zote zilizomo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anataka kujua juu ya watumishi 18 ambao hawajalipwa mafao. Nataka nimwombe

Mheshimiwa Mbunge kwamba watumishi hao kama hawajaleta barua katika Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi basi barua zao zifike haraka na kama wameshazileta baada ya hapa naomba nipate taarifa zaidi ili niweze kuyafatilia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Serikali mwaka jana ilipandisha vyeo au madaraja watumishi katika sekta ya umma baada ya kushindwa kupandishwa kwa takribani miaka mitano. Upandishwaji huu umesababisha changamoto ya walioajiriwa mwanzo na walioajiriwa baadaye wote kujikuta wapo katika kundi moja au daraja moja. Nini tamko la Serikali kutoa maelekezo kwa mamlaka za ajira nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili ifanye uchambuzi na hatimaye walioajiriwa wakiwa daraja moja waweze kuwekwa katika madaraja stahiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Kassinge Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba kuwapandisha vyeo watumishi ni sehemu ya kuwapa motisha ili waendelee kufanya kazi vizuri pia ni eneo la kuendelea kusimamia usimamizi wa watumishi wa umma katika nchi yetu. Nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hapo mapungufu yaliyojitokeza katika utumishi ambayo yanahitaji watu wapandishwe vyeo yote tunayafanyia kazi na tutaendelea kutoa taarifa kadiri tunavyoendelea kupata nafasi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taarifa za watumishi wako zote ambao wana malalamiko kama hayo kupitia wewe tungependa tuzipate Serikali ili tuweze kuzifanyia kazi na kuweza kuwapatia haki yao wafanyakazi hao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Katika Halmashauri ya Mji wa Bunda kuna walimu takribani 28 wamekuwa wakikwama kupandishwa madaraja na ili hali kuna wenzao wamekuwa wakipandishwa madaraja kila mwaka walioajiriwa kwa mwaka mmoja. Tumelifuatilia suala hili wanasema tatizo ni mfumo na mimi nimechukua hatua ya kumpigia Katibu Mkuu Utumishi. Ningependa kujua ni lini sasa tatizo hili litaisha kwa hawa walimu 28 wa Halmashauri ya Mji wa Bunda ili waweze kupata haki yao kama wengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Serikali ni kwamba watumishi wote wanaostahili kupandishwa vyeo wapandishwe kwa mujibu wa taratibu kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi. Na hapa nakusudia na nimaelekezo ya Serikali, kwamba kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bunda Mji na viongozi wote katika Halmashauri nyingine zote Tanzania, maelekezo ya Serikali yako wazi na wayafate na kutotii maelekezo hayo ni kutotii uelekezo halali ya Mheshimiwa Rais, ambayo ameelekeza katika, alipokuwa anatoa maelekezo tarehe 19 Aprili, kwamba anataka wafanyakazi wote wanaostahili kupandishwa vyeo wapandishwe vyeo, wanatakiwa kufanyiwa *recategorization* wafanyiwe *recategorization,* lakini pia wale ambao kwa muda mrefu sana wamekuwa wanasubiri kuajiliwa nao pia wenye sifa za kuajiriwa, waajiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maelekezo haya yote nataka nikuhakikishie Bunge sisi kama Wizara au Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunayasimamia hayo na ni maelekezo yetu kwamba tunataka halmashauri zote nazo zisimamie na kama kuna sehemu yeyote pamekwama basi wawasiliane na Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi ili kuweza kushughulikia changamoto zitakazokuwa zimejitokeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe kauli ya changamoto kubwa iliyopo ya mfanyakazi anapandishiwa mshahara vizuri kabisa lakini harekebishiwi mpaka anastaafu, na inampa matatizo ya kupata haki zake. Mheshimiwa hii ni changamoto kubwa naomba Serikali itoe kauli yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Sitta Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwanza kulihakikishia Bunge lako lakini pia kumuhakikishia Mbunge ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunayo idara maalum inayohusika na masuala ya marupurupu, mishahara na nyongeza zote ambazo ni stahiki za mtumishi anatakiwa kupata. Sasa kama wapo watumishi ambao wanachangamoto katika hayo ofisi yetu iko wazi na ningeomba tupate taarifa hizo ili sasa tuweze kushughulikia na wafanyakazi wetu wote waweze kupata haki yao kama ambavyo imeelekezwa katika ratiba yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi hiyo hiyo Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Na. 625

**Likizo kwa wazazi wenye watoto njiti**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza siku za likizo kwa wazazi wanaojifungua watoto njiti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa likizo ya uzazi kwa watumishi kwa mujibu wa Kanuni H12 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 ambapo pamoja na Kanuni Pili ya Kanuni ya 12 inabainisha kuwa muda wa likizo ya uzazi kwa mtumishi mwanamke ni siku 84 ambazo hutolewa mara moja katika kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuongeza siku za likizo pale mtumishi anapojifungua mtoto njiti, suala hili halijawekewa utaratibu wa kikanuni kutokana na taratibu wa uendeshaji wa shughuli za Serikali. Hivyo, Mtumishi (Mzazi) anaweza kuomba ruhusa ya kawaida kutoka kwa Mwajiri wake inapotokea changamoto kama hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa nafasi hii nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sasa Serikali haioni kwamba kuna haja ya kubadilisha sheria iliyopo ambayo inawanyima haki watoto wale kwa sababu wanaachwa wakiwa wadogo sana, wachanga, kiasi kwamba inaweza ikawasababishia vifo kwa kukosa uangalizi wa karibu wa mama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, Serikali sasa haini kwamba kwa kumnyima hizo haki mama yule ambaye amejifungua mtoto njiti wa siku zile za nyongeza kunaweza kukamsababishia matatizo ya afya ya akili ambayo itagharimu tena Serikali kumtibia matatizo ya afya ya akili ambayo yatamfanya asifanye kazi yake ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kubadilsha sheria nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sheria zipo, miongozo ipo na taratibu zipo. Changamoto inayotokea labda ni ile ambayo naweza kusema kwamba kuna baadhi ya Waajiri ambao kwa roho mbaya tu wanaamua kuwanyima hawa wazazi wanaopata watoto njiti. Lakini kwa upande wa sheria na zote zimeelezwa wazi, na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako, lakini pia kutoa maelekezo kwa waajiri wote kwamba inapotokea mama amepata mtoto njiti na mazingira yanafahamika, watoto wanatakiwa kulelewa katika *kangaroo* basi ni wito wangu kwamba waongozwe pia na ubinadamu katika yale mamlaka ambayo wamepewa ili waweze kuwapa nafasi wazazi wakalee watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili katika maeneo ambayo kinamama *may be* labda wanakumbwa na hili tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliita kwamba tatizo la afya ya akili; nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali inayoongozwa na mwanamama Dkt. Samia Suluhu Hassan inawajali wakinamama Watanzania, inawajali watoto wa Tanzania lakini pia inatambua na kuheshimu na kulea afya za akili za Watanzania. Kwa hiyo nataka nikuhakikishie kwamba kama panapotokea matatizo hayo Mheshimiwa Rais ameishatoa maelekezo lakini pia na sisi tuwe chini yake tunamsadia, tumekwishapewa maelekezo na tunachotakiwa kufanya ni kuwaonea huruma wazazi hawa na kuwapa nafasi ili waende

wakalee watoto wao ambao wamezaliwa katika mazinguru magumu kama hayo yaliyotajwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENNEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yanayotolewa na Naibu Waziri, Ridhiwani Kikwete nimesimama kwa sababu ya uzito la suala la watoto njiti. Wazazi wao wanapotakiwa wakimaliza siku 84 katika likizo ya uzazi, na bila shaka wote tunakubaliana kwamba siku 84 kwa mtoto aliyezaliwa njiti anakuwa bado hajaimarika sawa sawa; na unjiti unatofautiana, wengine wanazaliwa na miezi sita, wengine wanazaliwa miezi saba, wengine wanazaliwa miezi nane wanakuwa hawajakamilika uumbaji unakuwa bado unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo chama/*NGO* inayohusiana na masuala ya kusaidia watoto njiti, wamekwishaleta malalamiko mengi sana Serikali. Sasa leo nataka nionyeshe mahala ambapo Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika kuona kama tunahitaji kweli kubadilisha sheria au sheria iliyopo inajitosheleza kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Kanuni za Utumishi wa Umma ya Mwaka 2009 Kanuni ya pili, H16 mnaweza mka-*google* hata nikimaliza kujibu swali mtapata maelezo yanayosema; "*Except in cases of illness or other cases of emergence*" yaani kwenye kesi hizi mtumishi ana haki ya kuomba *extension of leave*. Sasa tunajaribu kuona kama inatosha au haitoshi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kundi hili ni kweli mtu akizaliwa anapofariki inaumiza sana na wengi humu tumezaliwa tukiwa njiti. Hatujisemi tu humu lakini tusingeangaliwa kwa zaidi ya siku 84 tungekuwa hatupo leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuipitie hiyo Kanuni halafu Waheshimiwa Wabunge wale wenye maoni, watatuletea maoni kama inatosha au haitoshi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mheshimiwa Fatuma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa likizo ya uzazi ambapo wanaume wanapata siku tatu;

Je, Serikali haioni umefikia wakati kuongeza walau mwezi mmoja kwa wale wenza ambao watakuwa wamezaa watoto njiti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Toufiq Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake linaweza kuwa limejibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wakati anatoa maelezo ya ziada katika majibu yangu niliyompa Mheshimiwa Mtanda. Na mimi nadhani ili nalo tuliunganishe katika maombi aliyotoa Mheshimiwa Waziri la kutoa maoni ili kuona kama kuna sababu ya kurekebisha baadi ya vifungu vilivyomo katika sheria na kanuni inayoongozwa masuala yote ya likizo hasa pia kwa wanaume ambao Mheshimiwa Toufiq anawapigia debe waongezwe zifike siku 30. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru swali langu ndiyo hili la Mheshimiwa Toufiq kuhusiana na wanaume, nashukuru tumeishapata majibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na watoto njiti lakini pia kuna wanawake ambao wanajifungua watoto zaidi ya mmoja;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea siku akina mama hawa ili angalau waweze kuweza kuwalea vizuri hawa watoto mpaka wanapofikia umri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikiri mbele yako kwa kuwa mimi siyo mtalamu sana katika eneo hili analozungumza Mheshimiwa Mwaifunga, hasa anapofikia mama amezaa watoto zaidi ya mmoja au wawili au watatu kwa maana kwamba anahitaji kipindi gani ili aweze kupumzika. Lakini nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako, maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri yatioshe kufungua ili boksi la mjadala wa hii sheria na kanuni ili tuweze kuona jinsi gani tunaweza tukarekebisha hasa tukiweka *into consideration* mawazo mazuri ya Mheshimiwa Mbunge Hawa Mwaifunga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunashukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuendelea kuna matangazo ya wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Kwanza wageni waliopo kwenye Jukwaa wa Spika, wapo wageni saba wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Vijana wa Chama cha Mapinduzi Tawi la Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* UVCCM kutoka Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, ahsante karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Ndugu Patrick Gerald kutoka Jijini Mbeya, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 80 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Mbunge ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

ambao ni Baraza la Watoto la Taifa likijumuisha watoto wa Tanzania Bara na Zanzibar ambao wamekuja kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika na timu ya mpira wa miguu ya watoto wa kike za *African Lyon* ya Dar es Salaam na *Fountain Gate* ya Dodoma ambao ni Mabingwa wa Afrika, ahsante sana na karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni kumi wa Mheshimiwa David Kihenzile (Mbunge) ambao ni Umoja wa Vijana Wakotoliki kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Stella Manyanya (Mb), ambaye ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Monica Mbega kutoka Wilaya ya Nyasa, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo (Mbunge) kutoka Singida Kaskazini, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mwita Waitara (Mbunge) kutoka Tarime, ahsante na karibuni *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi (Mbunge) kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Maulid Salehe Ali (Mbunge) ambaye ni Mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Florent Kyombo (Mbunge) ambao ni wanafunzi wa Chuo cha St. Johns kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji (Mbunge) ambaye ni mtoto wake anaitwa Ndugu Yusuph Abdalla, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Kepteni Abbas Mwinyi (Mbunge) ambao ni walimu wa mazoezi ya viungo kutoka *Royal Village Gym* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Leah Komanya (Mbunge) ambao ni Wakuu wa Shule za Sekondari kutoka Jimbo la Meatu Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Mwenyekiti wa CWT Ndugu Robiri Zacharia, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 24 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo (Mbunge) ambao ni Wenyeviti wa CCM Kata kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa Ndugu Khalid Shekoloa, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Priscus Tarimo (Mbunge) ambao ni Viongozi wa Kanisa la *Kingdom of Heaven on Earth Mission Church* na *TENAKH FM Radio* wakiongozwa na Mchungaji Dkt. Peter Inkyera, Kiongozi wa Kanisa na Mkurugenzi wa *Radio TENAKH FM,* ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Daniel Awack (Mbunge), ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Karatu, Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Edwin Swalle (Mbunge) ambaye ni Rais wa *DARUSO* wa mwaka 2011/2012 kutoka Njombe, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma (Mbunge), ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kutoka Hanang, Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Maryam Omar Said (Mbunge) ambao ni familia yake wakiongozwa na mume wake Ndugu Suleiman Juma Khamis, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda (Mbunge) kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Minza Mjika (Mbunge) kutoka Meatu Mkoa wa Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Michael Kembaki (Mbunge) kutoka Tarime, Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo (Mbunge) ambao ni walimu kutoka Arumeru, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao viongozi wa watatu wa Chama cha Mapinduzi Tawi la Kibasila, Kata ya Upanga Mashariki, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 48 na walimu saba wa Shule ya Awali ya Msingi St. Gema Galgan kutoka Wilaya ya Kondoa, karibuni sana wanafunzi na walimu. *(Makofi)*

Tunao wajumbe 125 kutoka Jukwaa la Wazalendo Huru wa Jijini Dodoma, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanja na Biashara, namwita Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 626

**Mpango wa kuwawezesha na kuwainua kiuchumi wanawake wasiojiweza**

**MHE. MWANTUMU DAU. HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha na kuwainua kiuchumi wanawake wasiojiweza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusukuru kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha mifuko na programu za uwezeshaji kwa lengo la kuwawezesha na kuwainua wananchi kiuchumi wakiwemo wanawake wasiojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* imeendelea kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - Awamu ya Pili kwa kuhawilisha ruzuku ili kuwawezesha wananchi wasiojiweza ikiwemo wanawake kupata mahitaji ya msingi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kujiunga kwenye vikundi na kuanzisha shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwahimiza wanawake wasiojiweza kutumia fursa za uwepo wa mifuko na programu za uwezeshaji ili kuanzisha na kuendeleza biashara zao, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU. HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ya Serikali aliyoyatoa. Nina maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo *BBT* kwa vijana, Serikali ina mpngo gani wa kuja na *BBT* kwa wanawake wasiyosijiweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili je, Serikali haina umuhimu wa kuhakikisha mikopo hii inawafikia wanawake hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja ya changamoto tulizonazo ni kuona namna gani ya kuwawezesha wanawake wawe na kesho nzuri kama ambavyo kuna programu hii ya kesho nzuri kwa vijana kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili ni wazo zuri ili kuona namna gani tunawasaidia wanawake ambao ndio wana mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi hii. Nadhani kama Serikali tunachukua hili ili tuweze kuja na programu maalum yenye mlengo huo kwa ajili ya kuhakikisha wanawake wanakuwa na kesho nzuri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili, ni dhahiri kweli Serikali tumeshaona changamoto zilizojitokeza kwenye mifuko mbalimbali ikiwemo ile 10% ilikuwa inatengwa na Halmashauri kwamba ilikuwa haiwafikii walengwa wakiwemo wanawake kutokupata kwa wakati na mambo mengine mengi. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo tupitie upya namna ya kuhakikisha mifuko hii inawasaidia na hasa wanawake waweze kupata fedha zile kwa wakati, lakini kulingana na mahitaji yao. Sasa tunaangalia kwa namna ya pekee zaidi wanawake wasiojiweza ili waweze kupata mikopo au uwezeshaji huu kwa wakati kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, Serikali imefanya tathmini kujua kama majukwaa ya wanawake yanaleta tija katika wilaya zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukwaa haya ya wanawake katika mikoa yamekuwa na tija kubwa, kwa sababu ndio ambayo yamepelekea wanawake wengi kupata mikopo, lakini pia kuwa na elimu ya ujasiriamali katika maeneo tofauti tofauti. Changamoto tuliyonayo ni kuona sasa tunawezesha zaidi majukwaa haya ya wanawake ili kuweza kupata mikopo kwa wakati, lakini yenye kutosheleza mahitaji yao kadri ambavyo wanaomba. Kwa hiyo kuna tathmini ya kutosha ambayo tunaifanya ili kuona namna gani zaidi ya kuendeleza majukwaa haya ya wanawake katika mikoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomar, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza ambalo linasema hivi, kwa wale wanawake wanaofanya kazi maofisini, lakini kipato chao kidogo. Je, mnawawezesha vipi katika na wao kufanikisha masuala yao ya kuweza kujinyanyua kiuchumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli, kuna wanawake ambao wanafanya kazi maofisi lakini mishahara yao kidogo haitoshi na hii ni kwa watumishi walio wengi, Serikali na hata katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna programu mahususi na Serikali wanafanya kwa wakati fulani kuhakikisha wanawapa upendeleo maalum kuwakopesha wakati mwingine mikopo ambayo haina riba. Pia kupitia ajira hizi watumishi hawa huwa wanapata kipaumbele kukopa katika taasisi za fedha, lakini pia wanaanzisha vikundi au *SACCOS* ambazo zenyewe zinawasaidia kujiwezesha kiuchumi au kupata fedha za ziada kwa wanawake ambao

wanakuwa hawana uwezo au ambao mishahara yao ni kidogo katika maofisi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujua Serikali inawasaidiaje wanawake wa Mkoa wa Simiyu ambao hawajiwezi kiuchumi na ambao hawapo kwenye mpango wa *TASAF*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli, katika mikoa au majimbo mengi ikiwemo Simiyu kuna wanawake wengi ambao hawana uwezo, hawajiwezi, lakini hawako kwenye ule mpango wetu wa *TASAF*. Moja ya maeneo ambayo tunayaangalia sasa kama nilivyosema ni kupitia zile 10% ambazo tunaweza kuzifanyia kazi na kuunganisha baadhi ya mifuko ambayo ilikuwa haiwafikii walengwa, ili tuone hawa ambao hawako kwenye *TASAF* lakini wana uhitaji maalum kama swali la msingi ulilouliza waweze nao kunufaika na fedha hizi za Mifuko ambayo itawasaidia kuweza kuanzisha shughuli mbalimbali za kijasiriamali, lakini pia kuinuka kiuchumi katika shughuli zao za kila siku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naghenjwa, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kujua kwamba Wilaya ya Same ina madini mengi ya *gypsum* hasa kwenye Kata za Bendera na Makanya na kwa kujua kwamba gypsum inaweza kuwa na *products* nyingi ambazo zitatengeneza ajira kubwa katika viwanda hivyo. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia wananchi wa Wilaya ya Same kupata wawekezaji ili waweze ku-*process* ile *gypsum* wa-*add value*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Naghenjwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja ya maeneo ambayo tunayaangalia ni kuhamsisha uwekezaji katika sekta nyingi ikiwemo hii ya madini na hasa ya *gypsum* ambayo inatumika katika maeneo mengi kwenye ujenzi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake najua ndio wanashiriki sana katika shughuli za kiuchumi kama nilivyosema tutaona namna ya kukaa na Mheshimiwa Mbunge ili tuone kama kunakuwa na andiko kwa ajili ya Wilaya ya Same ambayo litavutia mahususi uwekezaji wa viwanda katika sekta hii kwa maana ya kuzalisha *gypsum* na shughuli nyingine za kiuchumi au viwanda vingine katika Jimbo la Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, *SIDO* imepotelea wapi kwa sababu kwenye Jimbo letu sijawahi kusikia *SIDO*, iko wapi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nijibu swali la Dkt. Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* bado ipo na inaendelea kufanya shughuli zake, changamoto tuliyonayo ni mtaji mdogo wa kuweza kutoa huduma kama ilivyokusudiwa na shirika letu la kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo Tanzania. Sasa tutakuja na sheria mahususi ili tuone namna gani ya kuiwezesha *SIDO* iweze kufanya shughuli zake kibiashara badala ya kutoa huduma ambayo inahitaji mtaji zaidi wa Serikali. Kwa hiyo

tunadhani huu utakuwa ndio ufumbuzi ili waweze kuendesha shughuli zao kibiashara ili kuwafikia wajasiriamali wengi na wenye viwanda wengi zaidi kadri ambavyo uchumi wa sasa unataka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Wilaya ya Chemba ni Wilaya ambayo ina maeneo mazuri na ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji, lakini bahati nzuri sana tupo katikati ya Barabara ya *c2c*. Wizara ya Uwekezaji ina mpango gani wa kuwekeza kwenye Wilaya ya Chemba ambayo iko karibu kabisa na Makao Makuu ya Nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Monni ni kweli Chemba ni sehemu ya kimkakati kwa sababu iko katika barabara Kuu tunasema *South – North Corridor* ambayo tunaamini sasa kwa kufungua njia hizi kutakuwa na fursa nyingi za uwekezaji katika maeneo ya Chemba kama ilivyo Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuwatafuta wawekezaji, lakini nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na halmashauri kuanza kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji ili tunapopata wawekezaji wasipate kikwazo kwa maana ya kupata ardhi ambayo iko tayari kwa ajili ya uwekezaji katika sekta mbalimbali katika Jimbo la Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante.  Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 627

**Ujenzi wa laini ya kusafirisha umeme kutoka Iringa – Sumbawanga**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa *KV* 400 kutoka Iringa, Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga utaanza pamoja na kulipa wananchi waliopitiwa na laini hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *KV* 400 yenye urefu wa kilometa 620 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2023 na kukamilika mwezi Septemba, 2025. Mradi huu unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na Nchi za Kusini mwa Afrika *(Southern African Power Pool)* na utagharimu jumla ya shilingi 1,380,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imetoa shilingi bilioni 16.43 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 6,500 wanaopisha mradi na kazi ya ulipaji fidia imekamilika kwa awamu ya kwanza ambapo wananchi 4,750 wamepokea shilingi bilioni 13.67 na maandalizi ya awamu ya pili yanaendelea na malipo yanatarajiwa kufanyika ifikapo Julai, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Manase, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali na kwa hatua iliyofikiwa na hii itapelekea kukwamua hata makampuni makubwa na viwanda vikubwa ambavyo vilikwama kufunguliwa kutokana na kukosa umeme mkubwa. Pia kuna vijiji kadhaa na vitongoji kadhaa ambavyo vimekosa umeme kutokana na kuchelewa kwa mradi huu vikiwemo Vijiji vya Kata za Ulenje, Kinyara, Vijombe, Swaya, Igale, Iwindi na Bonde la Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme kwenye Vijiji vya Ihango Kata ya Ulenje na Mina na Lusungo Kata ya Iwindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali ina mkakati gani wa kukwamua Mradi wa *REA,* awamu ya tatu, *round* ya pili, ambao umekwama kwenye Jimbo la Mbeya Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Oran Njeza kwa pamoja, kwa sababu yanahusu umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Njeza pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwamba Mradi wetu wa Kupeleka Umeme Vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa pili, utakamilika ifikapo Desemba. Vijiji aliyovitaja vilivyo katika kata hizo vyote vitakuwa vimepata umeme kufikia mwezi Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi anayepeleka umeme kwenye eneo la Mbeya Vijijini ni mkandarasi wetu *ETDCO* ambaye ni kampuni tanzu ya *TANESCO* na ameuliza ni jitihada gani zimefanyika kukwamua mradi kwenye eneo lake. Mkandarasi huyu sasa amewezeshwa zaidi na kampuni mama ya *TANESCO,* lakini na sisi kama Wizara tumeweka utaratibu mpya wa kusimamia miradi hii ikiwa ni pamoja na kuajiri vijana kwenye maeneo yetu ya majimbo, lakini kuajiri wakandarasi wahandisi wengi zaidi wa *REA* kwenye maeneo ya mikoa na kuweka ma - *group* ya kijamii ya *WhatsApp,* Waheshimiwa Wabunge

wameyaona. Tunaamini kwa njia hizi na jitihada ikiwemo na kulipa pesa kwa wakati, miradi hii yote ya *REA* iliyokuwa inasuasua, itakamilika kwa wakati ikiwemo kwenye eneo la Mheshimiwa Njeza ambapo mradi utakamilika ifikapo Desemba kupitia makandarasi wetu wa *ETDCO*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa namuita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini aulize swali lake.

Na. 628

**Fedha ya *CSR* kusaidia Halmashauri zinazozunguka mbuga na hifadhi nchini**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kusaidia Halmashauri zinazozunguka Mbuga/Hifadhi za Taifa kupitia *CSR* kutoka kwenye mapato ya utalii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia utekelezaji wa Sera ya Uwajibikaji Kijamii *(Community Social Responsibility - CSR)* Serikali inatekeleza miradi ya ujirani mwema kwa jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi za Wanyamapori za Jamii. Katika kutekeleza Sera hiyo, Halmashauri za Wilaya pamoja na jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa, zinanufaika na mapato yanayotokana na utalii ikiwemo kupatiwa miradi

mbalimbali ya kijamii inayoibuliwa na wananchi kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhakikisha Halmashauri za Wilaya pamoja na wananchi wanaopakana na maeneo yaliyohifadhiwa wananufaika kutokana na mapato ya utalii kupitia utekelezaji wa Sera ya Uwajibikaji Kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wizara na taasisi zake zinatekeleza miradi hiyo moja kwa moja badala ya kupitia halmashauri.

Je, hawaoni sasa ni muda muafaka fedha hizo zitengwe zipelekwe halmashauri ili halmashauri itekeleze kwa usawia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwenye Mkoa wa Kilimanjaro tumepitisha sheria kali sana za mazingira zinazozuia kukata miti kwa ajili ya kutunza mandhari ile na hali ya Mlima Kilimanjaro, jambo linaloleta usumbufu kupatikana kwa nishati ya kupikia kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Je, hatuoni sasa kwa Mkoa wa Kilimanjaro ni muda muafaka fedha hiyo ya *CSR* tuitumie kuwaletea wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro nishati mbadala ya bei nafuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ya fedha hizi ni kuhakikisha kwamba zinakwenda moja kwa moja kwenye *community,* kwa maana ya kwamba kwenye jamii. Hatuna shida na halmashauri

lakini tumeona fedha hizi bora ziende moja kwa moja kutoka kwenye taasisi husika kwenda kwenye jamiii moja kwa moja kwa sababu kwanza tumeona jamii iweze kujua mchango wa uhifadhi na vipi wanaweza kunufaika na maeneo yale yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili tumeona kwamba, miradi mingi imekuwa inasuasua, sasa tukaona tukizipeleka fedha moja kwa moja, miradi hii itapata kumalizika kwa haraka na jamii iweze kunufaika. Kikubwa zaidi tumeona miradi ambayo inahitajika ndiyo iende kwa jamii. Kwa hiyo kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba wazo lake sawa tunaweza kulichukua tukaona namna ya kulifanyia kazi, lakini kwa sasa tumeona bora fedha moja kwa moja ziende kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nimwambie kwamba, fedha hizi ziko kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo maji, umeme, zahanati na hata shule, lakini vile vile tu kwa kuwa sasa suala la nishati mbadala kwa sasa ni ajenda ya kitaifa, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili alilolishauri tunalichukua, tunakwenda kulifanyia kazi ili tuone namna ambavyo tunaweza tukachota fedha kutoka kwenye fungu hili na kuweza kushughulika na masuala ya nishati mbadala kwa sababu ndio ajenda ya Kitaifa, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba imekuwa ni moja ya chanzo cha migogoro mikubwa kati ya wananchi na taasisi za Serikali, lakini kutokushirikisha wananchi kupitia sera hiyo ya uwajibikaji kwa jamii imekuwa ni moja ya vyanzo vya migogoro hii. Je, Serikali inaweza ikatoa tamko ni kwa nini fedha za *CSR* hazijaenda kwa wananchi ambao wanapakana na Hifadhi ya Mikumi kwa miaka sita mfululizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, naomba kujibu swali hilo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la fedha hizi ambazo kama ambavyo tumeeleza zinazotoka kwenye taasisi zinazosimamia uhifadhi. Lengo na madhumuni moja kwa moja ziende kwa wananchi, lakini changamoto iliyokuwepo ni moja kwamba fedha hizi haziwezi kutosheleza kupeleka kwenye Halmashauri zote kwenye maeneo yote. Kwa hiyo nimwambie tu Mheshimiwa, moja ni kwamba tunawashirikisha na ndiyo maana tukamjibu Mheshimiwa pale kwamba fedha hizi ni bora ziende moja kwa moja kwa wananchi ili tuwashirikishe na tuweze kujua wanachokitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakapopata fedha, tutahakikisha kwamba kwenye Halmashauri yake na maeneo yake fedha hizi zinafika na zinatekeleza miradi ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Usonge, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya utekelezaji wa *CSR* kupitia Halmashauri. Kwa ushauri wangu, je, Wizara sasa haioni haja ya kuja na sheria na kanuni kabisa ambazo zitawa-*guide* watu wa hifadhi pamoja na wanaofanya shughuli za kiutalii zaidi ili lile suala la *CSR* liwe suala la kisheria kabisa? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ushauri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake tunauchukua na tutakwenda kuufanyia kazi. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za *CSR* katika Vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Selous vya Zinga Kibaoni, Mtepela, Namatewa pamoja na Ngarambi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha katika Halmashauri hizo na maeneo aliyoyataja zitafika cha msingi Mheshimiwa Mbunge awe na subira, tutafute hizo fedha ili tuone namna ya kuja kusaidia wananchi katika maeneo hayo na wao waweze kunufaika na uhifadhi, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lilikuwa linahusu mabadiliko ya kisheria na tayari Mheshimiwa Waziri amelijibu. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa waboreshaji wakubwa wa mazingira ni wanawake wakiwemo wanawake wa Kilimanjaro wnaaaouzunguka mlima; na kwa kuwa hawa watu wanaotoa *CSR* wankwenda zaidi kwenye miradi mikubwa wakiacha kugawa miche na kuhakikisha kuwa miche ile inatunzwa na kuweza kufikia katika hali ya kurudisha uoto wa asili. Je, ni lini sasa taasisi hizo ikiwemo *TFS* wataweza kushirikiana na wanawake wa Kilimanjaro ambao wana nia sana ya kuboresha mazingira hayo kutokana na jambo alilolifanya Mheshimiwa Rais la *Royal Tour* kugawa miche ya matunda na miche ya kuboresha mazingira na kurejesha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa umeeleweka, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna uharibifu mkubwa wa mazingira maeneo hayo hasa yanayozunguka Mlima wa Kilimanjaro. Uharibifu ambao unasababishwa na shughuli za kibinadamu na hapa tunataka tuchukue fursa hii tutoe maelekezo tuwaambie wananchi, tuwashauri sana, waache kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo haya zikiwemo za ufugaji na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutajitahidi tupeleke fedha kwa Mkoa huu wa Kilimanjaro, hasa kwa akinamama, lengo na madhumuni ikiwa ni kuweza kurejesha ile hali katika ule Mlima Kilimanjaro. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 629

**Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi - Nduguti**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Nduguti kwa kuwa ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Wilaya ya Mkalama ambacho kinajengwa eneo la Nduguti ni kituo cha Daraja B na ujenzi wake ulisimama ukiwa umefikia hatua ya lenta. Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilitenga kiasi cha fedha shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo hicho. Mwezi Februari, 2023 Serikali ilitoa shilingi 300,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kituo hiki kilikuwa na *plan* ya kuwa Kituo A na kilishajengwa msingi kwa ajili ya ghorofa na ghorofa hilo lingekuwa na nyumba juu kwa ajili ya *OCD.* Sasa kwa sababu wamebadilisha na kuwa Kituo B, Serikali sasa ina mpango gani wa kepeleka fedha kwa ajili ya kujenga nyumba pembeni kwa sababu, sasa nyumba haitakuwepo tena juu?

Swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gari la Polisi kwa sababu tuna shida kubwa ya magari katika Halmashauri ya Mkalama? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba kwa ajili ya Askari au Mkuu wa Kituo ni kweli kwamba, awali ilikuwa kiwe Daraja A, lakini Sera ya Jeshi la Polisi inatambua Kituo cha Polisi Daraja A ni kituo kikubwa akinachostahili kujengwa kwenye ngazi ya Mkoa kwa maana ya kuwa chini ya *Regional Police Commander (RPC),* lakini hivi vinavyotokea ngazi ya Wilaya vinapaswa viwe Daraja B. Kwa hivyo, nyumba ile itatengwa katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kutoka kwenye mfuko wetu wa tuzo na tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gari la Polisi, juzi nilijibu hapa kwamba, tumetenga bilioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya Polisi, magari haya yatakapopatikana, Wilaya ya Mkalama ni moja ya Wilaya itakayopelekewa gari na pikipiki kuwezesha shughuli za ulinzi na usalama wa raia. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Omar Said.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu na uchakavu wa ofisi za Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Je, ni lini Serikali itaanzisha ujenzi mpya kwa ajili ya ofisi hizi katika Mkoa huu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mpango wa kujenga ofisi zote za Makao Makuu ya Polisi ngazi ya Mkoa. Kwa hiyo, tumeanza na Kusini Pemba, hatua itakayofuata ni Kaskazini Pemba ili Mikoa yote iweze kupata vituo vya Polisi vyenye ngazi ya Mkoa kwa maana ya Daraja A. Kwa hiyo, uwe na subira katika miaka miwili ijayo kituo hicho pia kitakuwa kimejengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omary Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 2015 nilikuwa nikiomba tujengewe Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Kilindi. Naomba *commitment* ya Serikali juu ya ujenzi wa kituo hicho cha Polisi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu juu ya *commitment.*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kigua kwa uhakika kabisa kwamba, ni kipaumbele cha Wizara kupitia Jeshi la Polisi kwamba, Wilaya zote ambazo hazina vituo vya Polisi zinajengewa vituo vya Polisi. Nikupe *assurance* Mheshimiwa tutaangalia kwenye mpango wetu namna gani tunaweza tuka-*fast track* kutokana na majukumu muhimu ambayo Lindi inakabiliana nayo kwa maana ya uhalifu, mifugo, na kadhalika ili waweze kuwa na kituo cha polisi kumwezesha *OCD* kutimiza majukumu yake vizuri. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyohiyo.

Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu sasa aulize swali lake.

Na. 630

**Kuongeza fedha za ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilayani Kishapu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Wilaya ya Kishapu ni kituo cha Daraja B, na ujenzi wake umesimama ukiwa umefikia kwenye hatua ya umaliziaji. Tathmini kwa ajili ya kumalizia ujenzi imefanyika na kiasi cha shilingi 262,672,520 zinahitajika. Fedha hizo zimepangwa kutolewa kwenye mfuko wa tuzo na tozo katika mwaka wa fedha 2023/2024. Fedha zitakapotolewa ujenzi huo

utakamilishwa, ili wananchi wa Kishapu waanze kunufaika na huduma za Polisi kupitia kituo hicho. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa jitihada hizi ambazo imeweka mipango ya kuhakikisha kwamba, mwaka 2023/2024 ujenzi huu unakamilika.

Swali langu la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kuambatana na mimi ili kwenda kuona jitihada zilizofanywa na Mfuko wa Jimbo wa kwangu kama Mbunge, lakini nguvu za wananchi, wadau wa maendeleo kama Mgodi wa Mwadui Williamson?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri, utakuwa tayari pia kwenda kuona jitihada kubwa zinazofanyika za kupata eneo katika Mji Mdogo wa Maganzo, ili tuweze kujenga kituo kingine kwa sababu Kituo kile cha Maganzo ni chakavu na bado kinahudumia Kata tano, Kata ya Mwadui Luhumbo, Kata ya Mondo, Kata ya Songwa na Kata ya Maganzo yenyewe ili kwamba, tuone namna ya kuweza kuwapa huduma kwa usahihi na katika hali ya ubora wananchi wanaozunguka maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi anazofanya na wadau walioko Kishapu katika ujenzi wa vituo vya Polisi kwa ajili ya usalama wa mali za wananchi na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utayari wangu kuongozana nae, Mheshimiwa nimeshakuahidi na hapa ninathibitisha kwamba, baada ya kumaliza Bunge letu hili mwezi Julai nitakuwa

tayari kwenda Kishapu, pamoja na mambo mengine, kuona jitihada za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini njambo la pili, tunatambua kweli katika Mji Mdogo wa Maganzo kuna shughuli nyingi za kibiashara na huko kwenye Mgodi muhimu wa Mwadui wa madini ya Almasi. Tunatambua uchakavu wa kituo kilichopo na kwamba kimebanwa sana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naweza nikashauri mapema kabla sijaja huko, ni kupata eneo ili tukiona kwamba eneo hilo linatosha tuliingize kwenye mpango wetu wa kujenga kituo kinachostahili kwenye eneo hilo la Maganzo. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Siha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nikijibu hapa, kwa maeneo ambayo tumeona jitihada za Halmashauri na wananchi katika ujenzi wa vituo vya polisi ni kipaumbele cha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Jeshi la Polisi kuwaunga mkono ili kukamilisha. Tutaangalia katika mipangilio yetu namna ambavyo tunaweza tukapata fedha kupitia ama vyanzo vya fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu au fedha za tuzo na tozo kuwaunga mkono wananchi wa Siha kukamilisha kituo chao cha Polisi, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Goba, Mtaa wa Tegeta A wameweka nguvu zao nyingi sana kujenga Kituo Polisi chenye hadhi ya ghorofa moja kuungana na nguvu za Mbunge Mfuko wa Jimbo. Je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kuja Kibamba kuona ile kazi kubwa iliyofanywa na wananchi wale wa Tegeta A juu ya ukamilishaji wa kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari. Kwa juhudi zinazofanywa na Mheshimiwa Mtemvu na wananchi wake na wadau wengine katika jimbo lake niko tayari kwenda kushuhudia jitihada hizo na kuelekeza kuwaunga mkono kutoka Jeshi la Polisi ili kukamilisha vituo ambavyo tayari wameshavianzisha kwenye Jimbo lake, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tanganyika hatuna kabisa Kituo cha Polisi, lakini wananchi wa Wilaya hiyo wameonesha juhudi kwa kuanzisha ujenzi wa kituo cha polisi kwa kujenga msingi. Je, ni lini Serikali itaunga juhudi hizo kwa kutupatia pesa ili tuweze kukamilisha kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi Mheshimiwa Mariki kwamba, tunatambua umuhimu wa kuwa na Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya na vituo vingine kwenye Tarafa husika katika Wilaya ya Tanganyika. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge, tumeshaongea hata na Mbunge wa Jimbo kwamba, kwenye bajeti yetu ijayo tutaona uwezekano wa kuwachangia ili waweze kujenga kituo hicho, tumuombe Mwenyezi Mungu liwezekane liweze kutekelezwa, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari baada ya Bunge hili kufanya ziara kuja kuangalia nguvu za wananchi na Mbunge katika ujenzi wa Kituo cha Polisi kwenye Kata ya Nyijundu, Wilayani Nyang'hwale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuahidi nikitoka Shinyanga kwenda Nyag'hwale ni karibu sana, kwa hiyo, wakati namaliza ziara yangu Shinyanga pale Kishapu, kituo kitakachofuata ni Nyag'hwale ili kuona juhudi za wananchi hatimaye tumuunge mkono Mheshimiwa Mbunge. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 631

**Upanuzi wa njia nne Tengeru**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Tengeru utaendelea ikiwa ni mwendelezo wa barabara ya Sakina – Holili?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kuendeleza ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Tengeru kwa kutumia fedha za mkopo nafuu kutoka Shirika la Maendeleao la Japan *(JICA)*. Ujenzi utahusisha sehemu ya barabara ya Tengeru – Usa River yenye urefu wa kilometa 9.3, sehemu ya Moshi Mjini yenye urefu wa kilometa 8.4 na ujenzi wa daraja jipya la Kikafu lenye urefu wa mita 360. Kwa sasa mchakato wa manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya kazi ya usanifu wa kina wa barabara na daraja upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa usanifu, kazi ya ujenzi itaanza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pallangyo umeridhika? Swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara za lami huwa unaboresha sana mazingira na mandhari ya nchi yetu kule inakopita. Barabara hii pale inapoanzia kuna soko la Tengeru ambalo hali yake ni mbaya kimazingira na miundombinu, lakini tunajua kwamba, miradi mikubwa hii ina-*component* ya *CSR*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Halmashauri ya Meru kuboresha soko hili kwa kutumia *CSR* yake?

Swali la pili, kwa kuwa, mradi huu uko kwenye hatua ya usanifu na upembuzi yakinifu, Serikali haioni ni busara kuweka uboreshaji wa soko hili katika usanifu huo? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye miradi hii mikubwa kunakuwa na *component* ya *CSR*. Ninachoweza kumuomba Mheshimiwa Mbunge, tumelipokea ombi lake la kuboresha hiyo miundombinu ya soko la Tengeru pamoja na barabara inayoingia, lakini tu pengine nishauri ni vyema tukapata maombi rasmi ili tuweze kuyaratibu kabla Mhandisi Mshauri hajakamilisha, basi iwe ni sehemu ya mpango wa kuijenga hiyo barabara ikiwa ni pamoja na kujenga hiyo barabara ndogo ya kuingia kwenye soko na kuboresha hilo soko, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itajenga barabara ya Singida – Sepuka – Ndago kwa kiwango cha lami ambayo kimsingi ni barabara muhimu sana kwa wananchi na wakazi wa Tarafa ya Sepuka, Jimbo la Singida Mashariki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ya Singida – Sepuka – hadi Ndago ni barabara ambayo tunategemea muda wowote kusaini mkataba kwa ajili ya kuanza ujenzi kwani tayari taratibu zote za manunuzi zimeshakamilika. Kwa hiyo, kinachosubiriwa tu ni kuisaini ili ujenzi uanze kujenga barabara hiyo yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini barabara nne zitajengwa eneo la Nyangole, Bukoba Mjini ili kutimiza ahadi ya Makamu wa Rais?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nne eneo la Nyangole, ambayo iko Bukoba Mjini ilikuwa ni ombi la Mheshimiwa Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Byabato, wakati Makamu wa Rais amefanya ziara katika Mji wa Bukoba. Ninamshukuru kwanza Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge, kwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Oliver pamoja na Mheshimiwa wa Bukoba Mjini na wananchi wa Bukoba Mjini agizo hilo tayari tumeshaanza utekelezaji. Katika hii barabara tutafanya kazi tatu, moja itakuwa ni kuondoa, kupunguza zile kona, kupunguza mteremko, lakini pia kujenga barabara ya njia mbili zinazoshuka na njia mbili zinazopanda, tutaanza na kilometa nne, lakini mpango ni kujenga kilometa tano kutoka hapo Nyangoya hadi Bukoba bandarini. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba marekebisho kwamba, barabara ni ya kutoka Kibada hadi Tundwi, Songani, siyo kama ilivyoandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho haya. Naomba sasa swali langu Namba 632 lipatiwe majibu.

Na. 632

**Ujenzi wa barabara ya kutoka Kibada – Tundwi - Songani kwa kiwango cha lami**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Kibada – Tundwi hadi Songani kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee marekebisho ya Mheshimiwa Mbunge aliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Dar-es-Salaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kibada – Tundwi, Songani, Kimbiji yenye urefu wa kilometa 41 ambapo kwa sasa upo kwenye hatua za mwisho za manunuzi ya kumpata Makandarasi atakayetekeleza ujenzi wa mradi huu. Mkataba unatarajiwa kuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi huu Juni, 2023. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyogeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, barabara hiyo ya Kibada hadi Tundwi - Songani inakwenda mpaka Pemba Mnazi ambapo kuna viwanja vingi vimetengwa na Serikali, lakini kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa Barabara. Ukosefu wa kujengwa barabara hiyo unasababisha kuongezeka kwa nauli kwa wananchi wa Kisarawe II, Mwasongwa na Tundwi - Songani.

Je, nataka *commitment* ya Serikali, ni lini? Je, ni kweli itaanza kujengwa barabara hiyo mwezi Juni, maana imekuwa ni ahadi ya muda mrefu.

Swali la pili, changamoto ya ukosefu wa barabara inaikumba pia Halmashauri ya Ubungo. Barabara ya Victoria –

Mbezi – kwa Yusufu hadi Mpiji Magohe. Ni lini barabara hiyo nayo itajengwa?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali la kwanza la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, barabara hii niliyoitaja tunakwenda kuijenga, ndiyo maana bila kusita tunategemea mwezi kabla haujaisha huu wa Juni tuwe tumeisaini kwani Mkandarasi alishapatikana tuanze ujenzi wa barabara hii. Tunatambua umuhimu wa barabara hii kwani sasa limekuwa ni eneo muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa Dar-es-Salaam na hasa Jimbo la Kigamboni. Pia ni kwamba, tunajua alikuwa amepata changamoto ya kuharibika, Mkandarasi tayari yupo *site* kuanzia Mji Mwema, Kimbiji lakini Mji Mwema - Mwasonga hadi Kimbiji kuhakikisha kwamba, anarudisha barabara kwenye hali yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara alizozitaja hizi tayari, kama ataangalia kwenye bajeti za Jimbo la Ubungo, barabara hizi tumeziingiza kwenye mpango. Kulikuwa na barabara moja ilikuwa haijafanyiwa usanifu hasa ile ya Kwa Yusufu - Makabe, lakini barabara nyingine hizi tumeziweka kwenye mpango wa kuanza kuzijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu ni muhimu sana inayounganisha Mkoa wa Manyara na Wilaya za Mbulu na Mji wa Arusha: Je, kwa nini Serikali imeshimdwa kutekeleza eneo la mlima Magara ambalo lina jiografia ngumu sana na inatumia gharama kubwa kwa kiwango cha changarawe? Lini itaweka lami mlima Magara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara hadi Mbulu ni barabara ambayo inapita kwenye *escarpment*. Mheshimiwa Mbunge atakuwa ni shahidi kwamba tunachokifanya sasa hivi, ni kukamilisha eneo lote la ule mwinuko kujenga kwa kiwango cha lami au kiwango cha zege. Baada ya kukamilisha hayo maeneo ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa, mpango sasa ni kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami, kwani usanifu tayari umeshafanyika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi katika swali hili ambalo limetoka kwa Mheshimiwa Mariam Kisangi, umesema kwamba barabara ile inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami, tunashukuru kwa hilo, lakini barabara hii kwa sasa hivi imeharibika sana kutokana na uzito wa magari yanayopita pale pamoja na mvua ambazo zimenyesha: Ni lini ukarabati wa barabara hii utafanyika wakati tunasubiri barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara nyingi za Dar es Salaam, hasa ambazo ni kwa kiwango cha changarawe, zimepata changamoto kutokana na mvua ambazo zimekuwa zinaendelea kunyesha katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini nataka

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika barabara zake hizo alizozitaja, tayari tumesham-*engage* Mkandarasi, *Ibra Construction Company* ambaye amepewa barabara ya kutoka Mji Mwema kwenda Kimbiji na pia huyu huyo atafanya kazi kutoka Kibada – Mwasonga – Kimbiji na kuendelea mbele ili kurejesha mawasiliano na kuondoa changamoto ambazo zinaendelea kwa sasa. Kwa hiyo, mkandarasi tayari ameshakuwa *site*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Kibiti wamenituma niulize kwa mara nyingine tena, ni nini mpango au mkakati wa Serikali kuhusiana na barabara ya Kibiti – Dimani mpaka Mloka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijampata vizuri kwenye majina ya ile barabara aliyoitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, rudia majina kwa kifupi.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naizungumzia barabara ya Kibiti – Dimani kwenda Mloka kule kwenye ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii sasa hivi tunairudisha tena kuifanyia *review* ya usanifu, lakini naamini ndiyo barabara ambayo tayari tunajenga lile Daraja kubwa la Mbambe kuhakikisha kwamba tunaondoa hiyo changamoto. Mpango ni kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ambayo pia ni barabara fupi sana kwenda Bwawa la Nyerere ukitokea Pwani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya milimani ya Vudee ni fupi sana, lakini kila mwaka Serikali inamwaga kifusi na mvua inaponyesha, basi inazolewa na maji: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kwamba tukimaliza Bunge twende Vudee milimani ili akaone barabara hii inayokwenda mpaka Ndolwa ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami au zege ili Serikali isipoteze fedha?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubalina na Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo ya milimani kwa kweli yana changamoto kubwa. Kwanza nitoe maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro aitembelee hiyo barabara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge twende tukaipitie, lakini twende wakati mtaalam ameshapita ili tuwe tayari tuna taarifa za awali kuhusu changamoto ambazo ziko kwenye hiyo barabara. Kwa hiyo nakubali, tutakwenda kuitembelea hiyo barabara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Watu wa Tarime wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama wa Taifa, kwa kutoa fedha ya kujenga lami kilometa 25. Sasa naomba nijue: Lini kipande cha kitoka Kwinogo – Nyamongo hadi

Serengeti Mugumu kitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tulishaongea na Mheshimiwa Mbunge, na kweli kipande hicho tutakijenga kwa kiwango cha lami. Tayari mkandarasi alishapatikana, taratibu za manunuzi zimeshapatikana. Tunachofanya sasa katika maandalizi ni kutafuta siku ya kusaini kipande kilichobaki cha kutoka Nyamwaga hadi Mugumu - Serengeti kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali hili hili ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Vijijini, nimeuliza mara nyingi na ni mara nyingi nimeongea na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu barabara hii ya Nyamongo mpaka Mugumu: Sasa tunaomba kujua ni lini hasa kwa maana ya tarehe, utakaposainiwa huo mkataba na kuanza ujenzi wa barabara ya Nyamongo – Mugumu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi, tarehe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge, na hasa Mbunge wa Tarime na Mbunge wa Serengeti, hii barabara inaunganisha Serengeti na Tarime, lakini kutoka Serengeti pia inategemea kwenda Nata. Naomba wawe na Subira. Taratibu zote za manunuzi zimeshakamilika, tunachosubiri ni kutafuta siku maalum ya kufanya *signing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna hakika, kama utaratibu utakwenda kama tulivyopanga ni kuisaini hiyo barabara

kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, siku itakapokuwa tayari, tutawajulisha Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti na Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Vijijini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika Chalinze kuna *roundabout* nzuri kuliko *roundabout* yoyote hapa nchini, lakini pale kuna kilometa 25 kufika Magindu: Ni lini barabara ile itajengwa kwa kiwnago cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tushukuru kwamba *keep left* ile ni kati ya *keep left* nzuri katika nchi yetu. Hiyo barabara aliyoitaja ya Chalinze – Magindu katika bajeti inayokuja imepangwa ifanyiwe usanifu yakiwa ni maandalizi ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sisi tuna barabara ya kutoka Namtumbo – Mtonya – Mgombasi, kuna daraja katika Mto Luwegu ambalo linahatarisha maisha ya watu, kwani ni jembamba sana: Je, Serikali inaweza kuiwekea fedha kulijenga daraja hilo ili kuepusha maafa yanayoweza kutokea? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nipokee ombi la Mheshimiwa Mbunge kwa sababu daraja hilo linahatarisha maisha ya wananchi. Pia nimwelekeze Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Ruvuma ili aiangalie hiyo barabara kwa maana ya Namtumbo – Mto Luwegu hadi Mgombasi, pia akaangalie daraja hilo, afanye tathmini, halafu alete Makao Makuu kwa ajili ya kutafuta fedha kulijenga hilo daraja la Mto Luwegu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Serikali imejenga madaraja mazuri kwenye barabara ya Lupila kwenda Ikonda: Je, lini mtajenga kwa kiwango cha lami ili kukamilisha kazi ile nzuri na wananchi wetu wakaweza kupita vizuri kwenye barabara ile? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia kule mwishoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, hujasikika, naomba urudie swali lako kwa ufupi.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imejenga madaraja mazuri kwenye barabara ya kutoka Lupila – Ikonda: Je, Serikali itajenga lini barabara ile kwa kiwango cha lami ili kuweza kukidhi matakwa ya wananchi wa Jimbo la Makete?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kujenga hizi barabara kwa kiwango cha lami. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa tumeshaanza kujenga hii barabara nzuri, tutahakikisha tunaifikisha mwisho ikiwa ni pamoja na barabara aliyoitaja kuijenga kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent.

**MHE. PROF KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Barabara ya Kimara – Mavurunza mpaka Segerea imewekwa kwenye bajeti ya mwaka huu, lakini kwa sasa haipitiki, hali yake ni mbaya sana: Kwa nini Serikali isifanye matengenezo wakati tukisubiri ujenzi wa lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, barabara za Dar es Salaam nyingi ambazo siyo kwa kiwango cha lami ziko kwenye mazingira magumu. Nimwagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam, aende kwenye barabara hii ambayo inaunganisha Jimbo la Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na Mheshmiwa Bonnah, waende wakaiangalie ili waweze kuondoa hizo changamoto na waweze kurejesha usafiri kati ya hayo majimbo mawili, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Serikali ya Awamu ya Tano iliahidi kuwajengea wananchi wa Minziro barabara ya kutoka Mutukula kwenda mpaka Minziro, na ni faraja kwamba Naibu Waziri alikuja akatembelea barabara hiyo na sasa hivi imeanza kufumuliwa: Je, lini sasa barabara hiyo itakamilika kwa kiwango cha lami kutoka Mutukula kwenda Minziro?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, barabara hii tulitembea na Mheshimiwa Mbunge, mimi nilishaitembelea. Kitu cha kwanza kilikuwa ni kuifungua hiyo barabara, na kitu cha pili tutakachofanya sasa ni kuifanyia usanifu. Ni barabara muhimu kwa sababu ipo kwenye uchumi na pia ni barabara ya ulinzi ambayo ni moja ya vipaumbele vya kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwa mujibu wa sera zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kuifungua yote tutaifanyia usanifu ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, sasa aulize swali lake.

Na. 633

**Ujenzi wa minara ya simu – Mbarali**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu maeneo yasiyo na mawasiliano hususan Kata za Ipwani, Miyombweni na Igava?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilibaini changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali yakiwemo Ipwani, Miyombweni na Igava ambapo Serikali imempata mtoa huduma wa kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata ya Ipwani kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali. Aidha, Kata za Miyombweni na Igava zitaingizwa katika miradi itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, hususan katika kata hizi tatu, lakini nina swali dogo la nyongeza: Je, Serikali iko tayari kupeleka mawasilino katika maeneo mengine yenye shida kama vile Ihahi, Azimio Mswiswi, Mapula, Ilaji, Igalako, Uhambule, Chamoto, Mbaliro na Matebete? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja zina mitandao isipokuwa jambo ambalo lipo kwa sasa ni kwamba, unakuta kata moja ina mtandao wa Halotel lakini

wananchi wanahitaji Airtel, na kata nyingine wana Airtel lakini wananchi wanahitaji Vodacom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote Na. 11 ya Mwaka 2006 lengo lake lilikuwa kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya mawasiliano, hata angalau kwa mnara mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Sheria yetu ya *EPOCA* Na. 3 inampa Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni. Sasa ili tutatue changamoto ya kuwa na minara mingi ndani ya eneo moja na kuwa na utitiri ndani ya eneo moja, tumeamua sasa kuingia kwenye kanuni ambayo inaelekeza watoa huduma; cha kwanza tuwe na *infrastructure sharing,* maana yake tukiwa na mnara mmoja watoa huduma wote watakwenda kuweka huduma ya mawasiliano pale ili Watanzania wote waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumeliongeza kuhakikisha kwamba tuna-*share* ile *spectrum* (masafa), badala ya kila mtoa huduma kuja na masafa yake, basi tumeruhusu ambapo sheria hapo kabla ilikuwa inazuia, sasa tumeruhusu ili kuhakikisha kwamba Waheshimiwa wote wenye changamoto za mawasiliano tuweze kuwapatia huduma kwa urahisi bila kuleta utitiri wa minara ndani ya nchi yetu, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Iliwahi kuahidiwa hapa Bungeni juu ya kutupatia minara kwenye Kata za Maduma, Kitasengwa, Kasanga na Makungu na Kasanga kuna kituo cha afya: Je, lini Serikali itatimiza ahadi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa David Kihenzile, ameshaleta changamoto hii na tunafahamu kwamba eneo la Kasanga kuna kituo cha afya, na ili kuhakikisha kwamba kituo kile

kinafanya kazi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, ni lazima tufikishe huduma ya mawasiliano. Maeneo haya ya Maduma, Makungu pamoja na Kasanga tumeshaingiza kuhakikisha kwamba yanatekelezwa ili wananchi wa maeneo hayo wapate huduma ya mawasiliano, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata za Busale, Ibanda na Itope zipo mpakani sana mwa Malawi, na siku zote unapopita kwenye kata hizo mawasiliano yanapokwa na Wamalawi. Hata juzi Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Josephine Keenja, ameshuhudia hoteli zote zilizopo mpakani zilivyokosa wateja kwa kukosa mawasiliano: Je, ni lini sasa Serikali itatuondoa kwenye utumwa huo wa kubaki kama Wamalawi wakati sisi ni Watanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe, Mbunge wa Jimbo la Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwa na Mradi wa Tanzania ya Kidigitali, tulikuwa na mradi wa *special zones and boarders.* Mradi huu ulikuwa mahususi kwa maeneo ya mipakani, hasa kule ambapo kuna mwingiliano wa mawasiliano na nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba mawasiliano ni uchumi katika maeneo ya mpakani, tunafahamu mawasiliano ni usalama, lakini ni haki ya msingi ya kila Mtanzania kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuhakikisha kwamba wanapata mawasiliano. Kwa vile Mheshimiwa Mbunge amesema, basi tutatuma timu yetu tukajiridhishe tena kuona ni maeneo yapi ambayo yamebaki kuwa na changamoto hizo ili tuweze kuchukua hatua, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwa kuwa Serikali katika Jimbo la Kisesa ilishaahidi kujenga mnara katika Kata za Isengwa, Mbugabanya, Mwabusalu, Mwakisandu, Lingeka na Mwabuma: Ni lini Serikali itatimiza azma yake hiyo ili kuboresha mawasiliano katika kata hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Jimbo la Kisesa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge alileta kata sita ambazo zilikuwa na changamoto, na kweli nasi tukajiridhisha kuna changamoto hiyo. Baada ya kupitia na kuangalia bajeti yetu, Mheshimiwa Rais ameridhia kupeleka fedha za ujenzi wa minara katika Kata za Mwabuma, Isengwa pamoja na Mwabusalu ambapo watoa huduma wa Airtel na *TTCL* watakwenda kujenga. Kata nyingine ambazo zimebaki, tunazipokea kama Serikali, fedha zitakapopatikana tutahakikisha kwamba tunafikisha huduma ya mawasiliano, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kata za Mwabayanda, Kulimi na Kata ya Mwangonoli zote hazina kabisa mawasiliano ya simu. Je, Serikali ina mpango gani kuzipatia kata hizi mawasiliano ya simu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Ndaki Mbunge wa Maswa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, tumeziingiza kwenye awamu ya kufanya tathmini. Tumeshafanya awamu ya kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kutoka hapa hizi kata kwa ustadi kabisa tuzipitie ili tukaziingize katika utaratibu wa kuzifanyia tathmini na pale fedha zitakapopatikana tuhakikishe tunafikisha huduma ya mawasiliano katika kata hizi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tuna Mkongo wa Taifa. Sasa Serikali haioni kuna haja ya kufunga minara hii hasa pembezoni ili kupunguza mahangaiko ya watumishi wawe na utulivu huko pembezoni wafanye shughuli zao kule kule hata kama kusoma wasome *online*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliingia kwenye mpango wa kujenga Mkongo wa Taifa. Mkongo wa Taifa faida yake ni kwamba unaweza kupitisha *traffic* kwa wingi tena kwa kasi ya mwanga lakini vilevile lengo la kujenga Mkongo wa Taifa ni kuondokana na mifumo tuliyokuwa tunatumia zamani ya *microwave* lakini japo *microwave* kuna maeneo ambayo bado tunatumia. Lengo la kuwa na Mkongo wa Taifa ni kwamba baadae tutaunganisha minara ili kuhakikisha kwamba huduma inaweza kupatikana popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo makubwa ambayo tayari yameshafanyika, ambayo ni faida kubwa inayotokana na mkongo wa Taifa. Kwa sasa tuna vitu tunaita *telecentre*, *telecentre* hizi maana yake kuna maeneo ambapo mgonjwa

haitaji kufika Muhimbili anaweza akapatiwa huduma akiwa Bukoba, akiwa Kagera, akiwa Mtwara lakini ile taarifa yake ikasomwa Muhimbili kule kwa sababu ya uwepo wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaomba pia tupokee ushauri wako tutaendelea kuboresha kuhakikisha kwamba nchi yetu inazidi kuhakikisha kwamba mifumo yote na huduma zote zinatolewa kwa kidigitali kwani ndio msingi halisi wa uchumi wa sasa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Kalenga Kata za Masaka pamoja na Kianga zina changamoto ya mawasiliano kwa muda mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipokee changamoto ya mawasiliano hayo ili tuweze kukaa na kuweza kuyapitia vizuri lakini naamini kwamba katika kata zake, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuna minara tumempelekea katika jimbo lake na tunaamini kwamba kwa kiasi hicho kikubwa ni zaidi ya asilimia 70 ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hizi kata ambazo amezitaja tunazipokea kwa ajili ya utekelezaji, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba yako Chitete na kwa bahati mbaya eneo hili halijapitiwa na Mkongo wa Taifa hivyo kusababisha changamoto ya mawasiliano kwenye tarafa ya Kamsamba na tarafa yote ya Msangano. Je, ni lini tutachepushiwa Mkongo wa Taifa kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna njia tatu za kufikisha mawasiliano pale ambapo hatujafikisha Mkongo wa Taifa. Tunatumia *microwave* na pale ambapo *microwave* haiwezi kufikisha tunatumia *Virtual Satellite* lakini kwa sababu ni nia na dhamira ya Serikali kuhakikisha nchi yetu yote inafikiwa na Mkongo wa Taifa. Mpaka sasa tumeshafikia Mikoa 25 lakini baada ya kufika Mikoa 25 tutaenda sasa Wilaya kwa Wilaya na mpaka sasa tumeshajenga kilometa 8319 lakini vilevile katika bajeti ya miaka miwili iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Mheshimiwa Rais aliridhia fedha takribani bilioni 345 kwa ajili ya kufikisha Mkongo wa Taifa katika maeneo mbalimbali ambapo ni kilometa 4442 zinaenda kujengwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kwamba zikisha kamilika tutakuwa tumefikisha kilometa 12314 ambapo ni sawasawa na asilimia 85 ya utekelezaji na lengo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi kufikia mwaka 2025, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo namwita Mheshimiwa Rehema Migilla, Mbunge wa Ulyankulu sasa aulize swali lake.

Na. 634

**Ujenzi wa Bwawa Kijiji cha Ichemba – Ulyankulu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza: -

Je ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa katika Kijiji cha Ichemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Antony Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa ujenzi wa bwawa ambao upo katika Kata ya Ichemba, Wilaya ya Kaliua unategemewa kukusanya maji ya matumizi ya nyumbani, pamoja na umwagiliaji kwenye mashamba na unategemewa kunufaisha wananchi wapatao 18,000 wa Kata ya Ichemba na maeneo mengine ya Ulyankulu. Zabuni ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo imeshatangazwa na RUWASA na taratibu zingine zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itatenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ambayo zitatoa maji kwenye bwawa na kupeleka mashambani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru majibu ya Serikali. Bwawa hili la Chemba ni bwawa kubwa sana na likikamilika lina uwezo wa kwenda kuhudumia kata zangu tisa za Jimbo la Ulyankulu na bwawa hili lina maji mengi sana baada ya upembuzi yakinifu na tayari Serikali imeshatutengea milioni 750

kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Sasa Je, upi ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba maji haya yataendelea kutumika pia kwenye shughuli za umwagiliaji?

Lakini swali lingine la pili, Je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kuongozana na mimi ili Bunge linapokwisha hapa uende uone hali halisi ya bwawa hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ya kwamba kwa kutambua kwamba tunalo bwawa kubwa ambalo ni chanzo kizuri cha maji kwenye kilimo cha umwagiliaji, Serikali itahakikisha kwamba katika mwaka wa fedha ujao tunafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili maji yale pia yatumike kama sehemu ya kilimo na yaguse eneo kubwa zaidi ya kata tisa za Ulyankulu ili wananchi waweze kunufaika na bwawa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda jimboni kuangalia jambo hili pamoja na watalaam wetu ili kuweza kuharakisha zaidi ili wakulima wa Ulyankulu waanze kulima kupitia chanzo hiki cha maji kupitia mfumo wa umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia bonde la Kiru na Magara kwa ajili ya umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kiambatanisho namba tano cha bajeti yetu tuliyoisoma hapa ndani tumeyataja mabonde 22 moja kati ya mabonde yaliyotajwa ni mabonde ambayo Mheshimiwa Mbunge

ameyataja na yapo katika hatua ya mshauri mwelekezi hivi sasa akikamilisha kazi tunaanza ujenzi mara moja ili wananchi wa Mkoa wa Manyara waweze kunufaika na skimu hizi za umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngassa swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Jimbo la Igunga tuna skimu kubwa ya umwagailiaji ya Mamapuli iliyopo pale Mwanzugi na kwenye bajeti inayotembea, Serikali iliahidi kutupatia fedha. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ili kuboresha miundombinu kwa ajili ya kuwahudumia wakulima waliopo ndani na nje ya skimu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu hii ni kati ya skimu 42 ambazo tumezitengea fedha na nimtoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tutakamilisha yale ambayo tuliahidi ndani ya Bunge hili kuhakikisha kwamba skimu ile inafanya kazi na inarekebishwa ili wananchi waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji kupitia skimu hiyo.

**MWENYEKITI:** Kwenye Wizara hiyo hiyo sasa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 635

**Utafiti wa zao mbadala wa korosho Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kufanya utafiti ili kubaini mazao yanayoweza kulimwa na kustawi Mkoa wa Mtwara kama mbadala wa zao la korosho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeendelea kufanya utafiti katika maeneo ya Mtwara ili kupata mazao mengine zaidi ya korosho ambayo mkulima ataweza kuzalisha ili kuondokana na utegemezi wa zao la korosho pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kupitia TARI imeendelea kuhamasisha kilimo cha mazao ya muhogo, ufuta, karanga, alizeti, njugumawe, choroko, mbaazi, mtama na kunde ambayo tayari yamefanyiwa utafiti na kuonekana yanafaa kulimwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Mtwara. Aidha, Wizara imetoa elimu ya kilimo bora cha mazao hayo ikiwemo matumizi ya mbegu bora, udhibiti wa visumbufu (wadudu waharibifu na magonjwa), kupanda kwa wakati na matumizi sahihi ya mbolea kupitia mashamba ya mfano, radio za kijamii na televisheni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza nataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha unawapatia mbegu bora kwa ruzuku wakulima wa mazao haya mengine.

Swali langu la pili, nataka kujua kuna changamoto kubwa sana ya masoko hasa ya zao la muhogo pamoja na mbaazi wakulima wanalima lakini wanakosa masoko ya uhakika. Nataka kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha masoko ya mazao haya yanapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa mbegu kwa ajili ya wakulima kwa mfumo wa ruzuku. Sisi kama Serikali tuko tayari kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji wa mazao haya na pindi pale mahitaji yakiainishwa kupitia *TARI* na *ASA* tupo tayari kuwapatia wakulima

mbegu hizi katika mfumo wa ruzuku ili waweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko ya uhakika, nikianza na mbaazi, kwenye mbaazi tayari tumeshaingia makubaliano ambayo bado tuko katika hatua za mwisho na Serikali ya India ya kuchukua zaidi ya tani 150,000 na hivi sasa ninavyozungumza Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo yuko India kwa ajili ya kufatilia jambo hili hili kuhakikisha kwamba tunapata soko la uhakikia la wakulima wa mbaazi ili kuondokana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili pia kupitia *TARI* na *MDT* ambayo ni taasisi inayo jishughulisha na masuala ya masoko ya mazao, tumeendelea kutoa elimu na mafunzo juu ya matumizi ya ziada ya mbaazi ikiwemo lishe lakini pamoja na matumizi mengine ya viwanda kwa ajili ya kuongeza soko la zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muhogo tunao mkakati wa kitaifa wa kuendeleza zao la muhogo wa mwaka 2020 mpaka 2030 ambao ndani yake pia umeainisha mikakati mbalimbali ikiwemo kuwahusisha watu wenye viwanda kwa ajili kutengeneza wanga kupitia muhogo, *industrial of starch* wanaita ili tuongeze soko la muhogo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tupo katika mawasiliano na ubalozi wa China, Rwanda na Burundi kuongeza wigo mpana wa soko la muhogo ili kuwaondolea changamoto wakulima juu ya upatikanaji wa uhakika wa soko la muhogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA A. JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, Serikali imejipangaje kushajihisha, kuongeza uzalishaji wa mazao ya nafaka asilia kama fiwi, mtama, uwele, ufuta, dengu,choroko na mbaazi kwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kilimo hiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga kuanzisha kanda za kilimo Tanzania *Agricultural Growth Corridor* ambalo lengo lake kubwa ni kulima mazao kutokana na afya ya udongo itakavyoruhusu. Kwa hiyo, tunaendelea na kazi ya upimaji wa afya ya udongo, yale maeneo ambayo mazao uliyosema yanastawi tutayapa kipaumbele na tutatenga maeneo ili wakulima wapate maeneo ya kutosha na waweze kunufaika zaidi kupitia mazao hayo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Prof. Ndakidemi swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kugawa miche bora ya kahawa yenye ukinzani dhidi ya magonjwa sugu ya kahawa kwa wakulima wa Jimbo la Moshi Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mibuni tuliyonayo asilimia kubwa imeshakaa zaidi ya miaka 25 na hivyo kupunguza uzalishaji, hivi sasa Serikali kupitia *TAKRI* na wadau wengine kama bodi ya kahawa tutahakisha kwamba tunazalisha miche ya kutosha na hasa kupitia teknolojia ya chupa ili wakulima wengi zaidi wapate miche iwafikie kwa urahisi na waweze kuongeza uzalishaji ikiwemo wa kulima wa jimboni kwa Mheshimiwa Prof. Ndakidemi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Zao la pamba ni miongoni mwa mazao yanayofanya vizuri katika Mkoa wa Mtwara lakini zao hili limezuiliwa kulimwa Mkoa wa Mtwara kutokana na ugonjwa ambao upo kwenye zao la Pamba Nchini Msumbuji Jimbo la Kabodayogado. Je, ni lini Serikali itaondoa zuio hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunalo tishio la funza wekundu ambao wanapatikana katika nchi za Msumbiji pamoja na Zambia na maeneo mengineyo. Kwa sababu ya tishio hilo tumeendelea kuweka *quarantine* na tuna sisitiza tu wananchi wa Mkoa wa Mtwara kuendelea kulima mazao mbadala kama ufuta, korosho lakini kwa hivi sasa kwenye pamba tunayo changamoto kubwa na hatuwezi kuachia hivi sasa kwa sababu ya tishio la hao funza wekundu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njau swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na ucheleweshaji wa mbegu kwa wakulima na hivyo wakulima kukosa tija kwenye kilimo chao. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mbegu zinapelekwa kwa wakati ili waweze kulima kwa tija? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, changamoto kubwa ya upatikanji wa mbegu kwa wakati ilikuwa ni kwamba mzalishaji mkubwa wa mbegu *ASA* alikuwa na yeye alikuwa anategemea mvua kama ambavyo mkulima kuzalisha mbegu. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan tumetenga fedha kuhakikisha kwamba tunaanza kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yetu ya mbegu ili tuwe tuna uwezo wa kuzalisha mbegu mwaka mzima na wakulima wazipate kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia katika mashamba yetu makubwa nane ya awali tumeweka miundombinu *center* na *lateral pivot* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunamwagilia mashamba haya na mbegu zinapatikana kwa mwaka mzima na zitawafikia wakulima kwa wakati na msimu ukianza watakuwa nazo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nashukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza

Mbunge wa Viti Maalum litaulizwa na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

Na. 636

**Utatuzi wa changamoto ya maji Mlowo**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, ni lini changamoto ya upatikanaji maji Mji wa Mlowo itatatuliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua adha ya maji wanayoipata wakazi wa Mji wa Mlowo ambapo hali ya upatikanaji wa huduma hiyo ni asilimia 49. Katika kukabiliana na hali hiyo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali inatekeleza miradi mitatu ambayo ni Mradi wa Uboreshaji Huduma ya Maji Mlowo ambao umekamilika mwezi April 2023, na inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Mtandao wa maji Vwawa-Mlowo na Mradi wa Ukarabati wa Chanzo cha Maji Mwansyana na Mlowo. Miradi hii inatarajia kukamilika mwezi Septemba, 2023 na kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Mlowo kufikia asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imepanga kujenga miradi mingine miwili ambayo ni Mradi wa Maji kupitia chanzo cha Mto Mafumbo, na Mradi wa Maji wa Vwawa-Mlowo na Tunduma kupitia chanzo cha Mto Momba. Miradi hiyo ipo kwenye hatua ya manunuzi ya Wakandarasi na ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili. Kukamilika kwa miradi hiyo kutawezesha wakazi wa

Mji Mlowo kupata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nataka nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri, Je, yupo tayari kuongozana na mimi Mbunge wa Jimbo la Mbozi kwenye mji wa Mlowo kuangalia hivyo vyanzo vya maji na kuhakikisha kwamba yote aliyosema yataenda kutekelezwa kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole Mbunge wa Jimbo. Awali ya yote nipokee pongezi lakini Mheshimiwa Mbunge na wewe nakupongeza na ninakusihi tuendelee kushirikiana. Ufuatiliaji wako wa karibu ndio matunda ya miradi hii kufika hatua hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongozana Mheshimiwa Mbunge, kama tulivyoongea ulipokuja Wizarani kufuatilia miradi hii, niko tayari na tutakwenda kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS STEPHEN CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Manyoni Mashariki kuna mradi wa maji wa Kintiko wa vijiji 11 Mkandarasi alisaini Mkataba mwezi Februari mwaka huu lakini mpaka sasa hivi kazi haijaanza. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba Mkandarasi anaanza kazi ya kumalizia huu mradi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Chaya Mbunge wa Jimbo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo anaongelea Mheshimiwa Mbunge ni kweli lakini nampongeza kwanza Mkandarasi ameanza kufanya kazi zile za awali na kinachosababisha hajaanza anasubiria *advance payment* lakini ninamsihi pale anapoweza kuendelea kufanya aendelee kwa sababu malipo haya yako mwishoni na yeye pia atalipwa kwa sababu tumeshapokea andiko lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali imenunua magari ya kuchimba maji katika kila Mkoa na yako chini ya *DDCA*. Je, ni lini yatakuwa chini ya Wahandisi wa maji wa Mikoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare kuhusiana na magari ya uchimbaji visima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sasa hivi magari haya yako chini ya *DDCA* tayari taratibu za ndani za kiwizara zinaendelea wakati wowote mambo yote yatakaa sawa kwa *RMs* wa Mikoa yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Wilaya ya Mbongwe ina maeneo yaliyo na changamoto ya maji. Je, ni lini Mbogwe mtatupa gari hilo la kuweza kuchimbia visima ili wananchi

waweze kupata maji safi na salama kupitia hayo, magari mliyoleta?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maganga Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavuyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Maganga anafatilia sana na hili tumeshaongea. Mheshimiwa Maganga naomba uiamini Wizara, mimi mwenyewe na wewe tutakwenda kuhakikisha kazi zinakwenda kuanza kwa wakati na visima vitachimbwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itatusaidia changamoto ya maji katika kata ya Kasokola katika Manispa ya Mpanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Kapufi kwa kweli umekuwa ukifuatilia kata hii na nikuhakikishie katika maeneo ambayo tunakwenda kupeleka jitihada ni pamoja na kata hiyo uliyoitaja kuhakikisjha wananchi nao wananufaika na hekima kubwa anayotumia Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha wanawake tunawatua ndoo kichwani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani kutuongezea visima virefu Mkoa wa Simiyu tukiwa tunasubiri mradi wa Ziwa Victoria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Esther Midimu kwa kweli naye pia ni mfatiliaji mzuri lakini nikupongeze kwa sababu ulishiriki katika usainishaji wa mradi ule mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria lakini masuala haya ya uchimbaji wa visima pia yatakwenda sambamba na maji kuvutwa kutoka Ziwa Victoria na visima hivi vyote mwaka ujao wa fedha tutajitahidi maeneo mengi kuyafikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Bupe Nelson Makang'ata Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 637

**Kukamilisha miradi ya maji Sumbawanga**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** atauliza: -

Je, ni lini mradi wa maji Kata za Kaengeza na Kanda Sumbawanga Vijijini itakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kaengesa ina vijiji vinne ambapo katika mwaka 2022/2023, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji Mkunda *Group* utakaohudumia vijiji vya Mkunda, Kaengesa A na Kaengesa B. Mradi huo unatarajia kukamilika mwezi Septemba, 2023 na wananchi Kijiji cha Mkunda wameanza kupata huduma ya maji. Kwa Kijiji cha Itela, Serikali itafanya usanifu na kujenga mradi wa maji katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata ya Kanda yenye vijiji vinne, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali

inaendelea kutekeleza mradi wa maji utakaohudumia vijiji vya Lula na Chitete. Vijiji vinavyobaki vya Lyapona A na Lyapona B usanifu utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024 na miradi kujengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, nilitaka kujua ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwenye mradi uliochukua muda mrefu mradi wa Inkana Isarye ulioko Nkasi Kusini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, nilitaka kujua ni lini sasa Serikali itakamilisha mradi wa kutoa maji katika Ziwa Tanganyika na kusambaza Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum kwa ufatiliaji wake mzuri na nipende kuhakikishia malipo ya mradi huu ambao umechukua muda mrefu ni mmoja wa vipaumbele vya Wizara kuhakikisha miradi yote inakamilika. Lengo la kupata maji bombani linatimia kwa sababu tunahitaji kuona tunapunguza umbali mrefu wananchi wa kutembea, vilevile kusambaza maji kutoka Ziwa Tanganyika ni moja ya vipaumbele vya Wizara. Mheshimiwa Bupe hili nalo pia Wizara tunalipa uzito na tutahakikisha maeneo yote ya Nkasi Kusini na Kaskazini kote tuweze kuyafikia na miradi iweze kukamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Jimbo la Njombe Mjini pamoja na kwamba linaonekana ni jimbo la mjini, uhalisia ni kwamba lina vijiji vingi sana ambavyo bado havina huduma ya maji kama Uliwa, Ihanga, Mikongo, Liwengi na Mtira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajaingizwa katika mpango mkubwa wa maji wa *P4R*. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba na vijiji hivi vinapata huduma hii ya maji safi na salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ni kweli. Mheshimiwa Mbunge nikupongeze hili mimi na wewe tumeshalijadili na tayari tumeanza kulifatilia. Maeneo ambayo hayata nufaika na mradi wa *P4R* ambao tunautekeleza kwa kutimiza vigezo vya masharti ya namna ambavyo unatekelezeka yatafanyiwa huduma kwa kupitia fedha za mfuko wa maji lakini vile vile fedha nyingine ambazo tunazipata kwenye namna nyingine ya upatikanaji wa fedha ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mbunge, nikuondoe hofu, kwa maeneo ambayo *P4R* haitafika haimaanishi hatutaweza kutekeleza miradi. Tutatekeleza miradi na wananchi watapata maji safi na salama ya kutosha na wote wataendelea kunufaika na kutuliwa ndoo kichwani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakukumbusha mradi wa maji wa Magugu - Mwada mpaka Minjingu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, ninayo matangazo machache.

Tangazo la kwanza ni wageni waliopo Bungeni muda huu; tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Mohammed Monni, Mbunge ambao ni walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Frolent Kyombo, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 54 na walimu sita wa Shule ya Msingi *Marangu Hills* kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wajumbe 125 kutoka Jukwaa la Wazalendo Huru kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 47 na walimu 10 wa Shule za Msingi *Martin Luther* ya Jijini Dodoma, ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Waziri Mkuu ambaye ni Mkuu wa Serikali Bungeni yuko nje ya Dodoma, hivyo Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma anakaimu nafasi hiyo ya kuwa Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kuwa tarehe 15 Juni, 2023 ni maadhimisho ya siku ya kuelimisha na kupinga ukatili dhidi ya wazee duniani ambao hufanyika kila mwaka. Lengo la maadhimisho hayo ni kuzingatia Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 66/167 la Disemba, 2021 lililotokana na maombi ya Shirika la Mtandao wa Kimataifa wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wazee. Kauli mbiu ya maadhimisho haya ni Wazee Wanastahili Heshima na Usikivu Wetu. *(Makofi)*

Aidha, maadhimisho hayo yatafanyika kimkoa na kiwilaya ambapo Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na wadau mbalimbali watajikita kwenye kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu masuala ya ulinzi kwa wazee dhidi ya ukatili.

Waheshimiwa Wabunge wote wanaombwa kushiriki katika maadhimisho hayo sambamba na kuhamasisha wananchi kwenye majimbo yao, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo machache, ninahairisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 5.43 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 15 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*